SportPesa
TZS. 710,494,580
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**Madaktari** kuchunguza athari mabegi ya wanafunzi

UKURASA 3



**Guardiola akunwa na kiwango akiivaa PSG**

UKURASA 23


# Nipashe

Ijumaa Novemba 26, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580776

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




# Samia atoa mwanga kwa sekta binafsi

• **Asema** wako katika mazungumzo na washirika...*Ukurasa 2*

## YALIYOMO

**UKURASA WA 4**

### TAZARA YASHTUKA MAITI KUTUPWA RELINI

MAMLAKA ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA), imeeleza kushtuka kuwapo kwa matukio ya mara kwa mara ya maiti...

## Serikali yaja na hatua sita kuzuia ukatili

UKURASA 3



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akionyesha mwongozo wa kushughulikia ukatili wa kijinsia katika vyuo vikuu na vyuo vya kati, baada ya kuuzindua sambamba na kampeni ya siku 16 za uanaharakati dhidi ya ukatili wa kijinsia, Dar es Salaam, jana. Kushoto ni Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mwanaidi Ali Khamisi na Mratibu wa Kitaifa wa Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Afrika (WiLDAF) Tanzania, Wakili Anna Meeda Kulaya. **PICHA: MIRAJI MSALA**

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe (kulia) na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Mafuta ya Total Energies, Jean-Francois Schoep, wakikata keki kuzindua vilainishi vipya vya magari na mitambo vya Total Energies, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mkurugenzi wa Sheria na Uhusiano wa kampuni hiyo, Getrude Mpangile. **Habari Uk.8. NA MPIGAPICHA WETU**



**KESI YA MBOWE**

## Shahidi adai alimkuta mahabusu shekhe mkoa

UKURASA 2

**MICHEZO** **SIMBA YAKAMILISHA 'MAWINDO'** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# Samia atoa mwanga kuiinua sekta binafsi




Rais Samia Suluhu Hassan, akifungua Mkutano wa 20 wa Taasisi za Kifedha Nchini jijini Dodoma jana, wenye lengo la kupitia na kutatua changamoto mbalimbali katika sekta hiyo. **PICHA: IKULU**

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan, amezitaka taasisi za kifedha nchini kutoa mikopo yenye riba nafuu ili kuiwezesha sekta binafsi kukua na kusaidia kukuza uchumi wa taifa ulioporomoka kutokana janga na UVIKO-19.

Mkuu wa Nchi pia amesema serikali yake iko katika mazungumzo na mashirika mbalimbali ili kupata mikopo ya fedha ambayo itatusaidia sekta hiyo na kuinua uchumi wa nchi.

Alibainisha hayo jana jijini Dodoma alipofungua mkutano wa 20 wa Taasisi za Kifedha nchini ulioandaliwa na Benki Kuu Tanzania (BoT).

Rais Samia alisema kufuatia janga na UVIKO-19, nchi nyingi duniani zimeporomoka kiuchumi kutokana na shughuli mbalimbali za uzalishaji mali kusimama.

"Ipo haja kama taifa kuona ni njia gani tunaweza kuzitumia kwa sasa ili kurejesha hali ya ukuaji wa uchumi wetu ulioshuka katika kipindi hichi cha janga la UVIKO-19.

"Katika kipindi hiki nchi yetu uchumi wake umeshuka hadi asilimia 4.8 kutoka asilimia 6.8 katika kipindi cha miaka mitano iliyopita lakini pia sekta ya Maliasili na Utalii ilishuka sana katika janga hili la UVIKO-19," alisema.

Rais Samia alisema kupitia mkutano huo wa 20, anatarajia washiriki kutoka na mapendekezo ambayo serikali itayatumia kurejesha hali ya kasi ya ukuaji wa uchumi kama ilivyokuwa awali.

"Niziombe taasisi zetu za kifedha kuhakikisha zinatoa mikopo kwa sekta binafsi ili kusaidia kukuza uchumi wa taifa ambao umeshuka kutokana na janga hili la UVIKO-19, kwani hivi sasa sekta binafsi bado haijachangamka kutokana na kukosekana kwa mikopo," alisema.

Vilevile, alisema serikali bado inaendelea na mazungumzo na mashirika mbalimbali ili kupata misamaha ya madeni ya mikopo.

"Pia tunaendelea na mazunguzo na mashirika mbalimbali ili kupata mikopo ya fedha ambayo itatusaidia 'kubalance' uchumi wetu," alisema.

Rais Samia alisema katika kukabiliana na janga la UVIKO-19, serikali imetekeleza hatua mbalimbali za kukabilina nalo ikiwa ni pamoja na kuchanja wananchi wake, hatua inayoendelea kufanyika nchini kote.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema juhudi zaidi zinahitajika kusaidia kurejesha hali ya ukuaji wa uchumi kama ilivyokuwa kabla ya janga la UVIKO-19.

"Benki zinatakiwa kuwa wabunifu kutusaidia kupata namna ya kutengeneza mipango ambayo itawasaida vijana kupata mitaji na tunawakaribisha kuleta kwetu maoni mbalimbali ili hadi tunakwenda bajeti ya pili tuwe na jambo la kisera ambalo tunaweza kulizungumzia," alisema Dk. Nchemba

Alimpongeza Rais Samia kwa jitihada zake alizozifanya ikiwamo kulipa madeni kiasi cha Sh. bilioni 22 kwa wazabuni ambao walikuwa wanatoa huduma katika shule na taasisi mbalimbali.

"Mheshimiwa Rais hawa watu walikuwa wengine wadai kwa miaka sita bila kulipwa na wengine walikutana na changamoto mbalimbali ikiwamo zile za kibenki lakini uamuzi wako uliwaokoa sana na kuwarejeshea amani waliyokuwa wanaikosa," alisifu.

Waziri huyo pia alitoa rai kwa Watanzania kuacha tabia ya kuhifadhi fedha ndani ya nyumba bali wazipeleke katika taasisi za kifedha ili kuongeza chachu ya kukua kwa uchumi.

Gavana wa BoT, Prof. Florens Luoga, alisema mkutano wa mwaka huu ni muhimu kwa sababu wadau wa sekta ya fedha wanaadhimisha miongo minne ya Mkutano wa Taasisi za Fedha tangu kuanzishwa kwake Mei 1980.

Alisema mkutano huo umekuwa jukwaa la wakuu wa taasisi za fedha, wasomi na watendaji kukutana na kujadili masuala yanayohusu maendeleo ya sekta za benki, fedha na uchumi kwa ujumla.

Alibainisha kuwa sekta ya utalii, ambayo imekuwa moja ya vyanzo vikubwa vya mapato ya fedha za kigeni, iliathiriwa zaidi na janga la corona kwa kuwa mapato yake yalipungua kwa zaidi ya nusu na kufikia dola za Marekani milioni 714.5 mwaka 2020.

"Hali hii ilitokana na kupungua kwa idadi ya watalii kwa asilimia 60 na kufikia 620,867.

"Aidha, ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi ulipungua hadi asilimia 4.3 mwaka 2020/21 ikilinganishwa na asilimia 8.1 mwaka 2019/20 kutokana na kushuka kwa mahitaji ya mikopo na kuongezeka kwa vihatarishi vya mikopo kwa wakopaji," alifafanua.

## KESI YA MBOWE

# Shahidi adai alimkuta mahabusu shekhe mkoa

**Na Kulwa Mzee**

MSHTAKIWA Mohammed Ling'wenya, ametaja mateso aliyopewa na polisi kutoka Moshi hadi Dar es Salaam na kudai kuwa katika Kituo cha Polisi Tazara, alikutana na Shekhe Mkuu wa Mkoa wa Manyara akiwa mahabusu na Luteni Denia Urio alimsikia na kumwona akilia kwenye magari mabovu yaliyopo nyuma ya kituo hicho.

Mshtakiwa huyo ambaye ni shahidi wa utetezi kwenye kesi ndogo alidai hayo jana Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi mbele ya Jaji Joachim Tiganga, akiongozwa na Wakili Dickson Matata kwenye kesi ya ugaidi inayomkabili Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe na wenzake watatu.

Shahidi alidai Agosti 5, 2020 walivamiwa na polisi zaidi ya wanane wakiwa Rau Madukani Moshi na kumkamata pamoja na Adamu Kasekwa na kuwapeleka mahabusu Kituo Kikuu cha Polisi Moshi.

Alidai kuwa aliingizwa kwenye chumba chenye watu wengi, wengine wakiwa na kamera, na kumuhoji kafuata nini Moshi na alipowajibu kuwa kafuata kazi ya ulinzi wa kiongozi kwa Mbowe, walisema anadanganya wanajua kafuata nini.

"Wakati huo nilifungwa pingu, Inspekta Mahita Omari akasema sitaki kusema, nitasema tu, alichukua bomba akapitisha kati kati ya miguu na mikono, nikabinuka wakati huo nyayo zikawa juu, alianza kunipiga sana, nililia, nilikuwa siwezi kuongea, nikasikia sauti ya askari akisema msimpige mwacheni, wakanishusha kisha wakanipeleka selo.

"Agosti 6, 2020 nilitolewa selo, ilikuwa jioni, nikafungwa kitambaa kizito nikapakiwa kwenye gari, sikuwahi kuzunguka mahali popote Moshi kwanza nilikuwa mgeni, nilitoka moja kwa moja kuletwa Dar es Salaam.

"Kwenye gari kabla sijafungwa kitambaa nilimuona afande Mahita, Goodluck na Jumanne, gari haikusimama mahali popote hata kukojoa, nilikuwa nimefungwa pingu, nimefungwa kitambaa, sikuruhusiwa kuinua shingo, nikiinua kichwa nakandamizwa kutoka Moshi hadi Dar es Salaam," alidai Ling'wenya.

Pia, alidai walipofika Dar es Salaam alishushwa na kuingizwa selo na kufunguliwa kitambaa, askari walipoondoka alijiburuza hadi mlangoni akaona mahabusu wengine chumba cha pili.

"Niliwauliza hapa wapi, wakasema Kituo cha Polisi Tazara, waliniambia Tazara wanawekwa wenye kesi za ugaidi, niliwaambia nilikuwa askari kikosi cha Makomandoo 92 KJ, niliyekuwa naongea naye alisema ni mwanajeshi kikosi cha Twalipo, alisema hakuna anayejua kama yuko Tazara.

"Alisogea mahabusu mwingine kwa mdomo wake alisema ni Shekhe Mkuu wa Mkoa wa Manyara," alidai.

Aliendelea kudai wakati analialia shida ya mahitaji kama mawakili alimuuliza Sajenti Kidume amueleze nini shida zake, askari huyo alimjibu awaulize wenzeke hapo ndiyo Tazara.

"Nilipopandishwa juu niliwaona madepo wenzangu niliokuwa nao Kikosini, Alex Ahadi na Chuma Chugulu, waliniambia hapa Tazara usiwe na wasiwasi.

"Nikiwa juu nilihojiwa vitu vingi, waliniuliza nani kanikutanisha na Mbowe, nikajibu Luteni Denis Urio ndiyo kanitafutia kazi ya kumlinda, nilihojiwa kama dakika 30 na Mahita kisha nikarudishwa selo sikutolewa tena tarehe 7 Agosti, 2020.

"Agosti 8 mwaka 2020 mahabusu wenzangu walinishtua wale jamaa wamefika, hawakufika kwenye chumba changu, walikuwa wanaongea na simu wakaenda nyuma ya kituo kwenye magari mabovu.

"Selo yangu nilikuwa naona nyuma, nilimuona afande Goodluck, Chuma Chugulu na baada ya muda nilisikia mtu analia kwenye magari mabovu, nilimtambua aliyekuwa analia ni Luteni Denis Urio.

"Namfahamu Urio Mwalimu wangu, niliwahi kufanya naye kazi 92 KJ, sikuona walichokuwa wanamfanya ila nilimuona wakati wanamtoa analia, kwa ufahamu wangu nikajua alikuwa anapigwa.

"Agosti 9, mwaka 2020 walinifunga kitambaa, wakanitoa selo na kunipeleka Kituo cha Polisi Mbweni, kule Mbweni nilibadilishwa jina nikaitwa Johnson John.

"Nikiwa napelekwa mahabusu kwenye korido nilipishana na Luteni Urio, nilisikia askari akisema mmoja ameletwa muda mrefu kasema ni Luteni.

"Nilitolewa mahabusu na kupelekwa kwenye chumba kiliandikwa ofisi ya Upelelezi, nilimkuta Goodluck kasimama mlangoni na bastola, afande Jumanne aliingia na bahasha ya kaki akatoa makaratasi huku akisema hatutaki usumbufu.

"Good luck alisema ukileta ujanja ujanja tutakufanyia kama Moshi, nilipata hofu nikasaini bila kusoma," alidai.

Aliendelea kudai mahakani hapo kuwa Mbweni mahabusu alikuwa na Luteni Urio na Kasekwa, lakini asubuhi alikuwa akimsalimia kwa kelele, Kasekwa alikuwa chumba kingine, lakini Urio hakuwa akimpigia kelele," alidai Ling'wenya.

Awali, kabla ya ushahidi huo upande wa mashtaka walifunga ushahidi baada kuleta mashahidi wanne mahakamani kupinga tuhuma za kumtesa mshtakiwa wa tatu Ling'wenya na kumsainisha maelezo ya onyo kwa vitisho.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Robert Kidando, aliieleza mahakama kuwa walifikia uamuzi huo baada ya kupitia Sheria ya ushahidi.

"Baada ya kupitia sheria ya ushahidi tunaomba kufunga ushahidi katika kesi ndogo," alisema Kidando na upande wa utetezi haukuwa na pingamizi.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni, Mbowe, Kasekwa, Ling'wenya na Halfani Bwire ambao wanashtakiwa kwa kula njama, kufanya vitendo vya kigaidi kati ya Mei mosi na Agosti 5, 2020.

## HABARI KITAIFA




Rais wa MAT, Dk. Shadrack Mwaibambe

# Madaktari kuchunguza mabegi ya wanafunzi

**Na Waandishi Wetu**

CHAMA cha Madaktari Tanzania (MAT) kimesema kinaanza utafiti kubaini athari wanazozipata wanafunzi wa shule za msingi ambao hukaa zaidi ya saa 12 shuleni na kubeba mabegi mazito.

Kimesema kimekuwa kikipokea maswali yanayohusu wanafunzi wa madarasa ya mitihani ya taifa, wakiwamo la nne na saba, kulazimika kupata masomo ya muda wa ziada au wanafunzi hao kulazimika kukaa bwenini.

Kutokana na hali hiyo, MAT imesema imepokea malalamiko kutoka kwa wazazi kuhusu hali hiyo, huku chama hicho kikisema kubadilishwa muda wa masomo uliopangwa na serikali, kunaweza kuchangia athari kiafya kwa mwanafunzi.

Rais wa chama hicho, Dk. Shadrack Mwaibambe, akizungumza na Nipashe juzi kuhusu suala hilo baada ya kutoa tamko lao, alisema wanaanza uchunguzi kubaini athari za kiafya kwa watoto kwa kuhoji wazazi na shule husika.

"Watoto kulazimika kusoma kwa muda wa ziada, kuishi bweni, kubeba mabegi mazito na kukosa muda wa kupumzika na michezo. Chama kina wajibu wa kikatiba kuishauri serikali juu ya mambo ya afya," alisema Dk. Mwaibambe.

Kadhalika, Dk. Mwaibambe alibainisha suala lingine ambalo ni usafiri binafsi wa gari la kuwafikisha shuleni watoto, hauzingatii kanuni za kiafya kutokana na wanafunzi kujaa kupita kiasi, huku wanafunzi wenye umri mdogo wakiathiriwa zaidi.

"Tunataka kujua ukubwa wa tatizo, ushahidi katika suala hilo na shule zinazofanya hivyo tuwe na mifano, tuzungumze na Waziri wa Elimu na kutoa ushauri wa kiafya juu ya afya za watoto," alisema.

Kiongozi huyo wa MAT alisema hivi sasa wamezipokea kero na taratibu hatarishi na kuzifanyia kazi ili kuishauri serikali kwa kuwa muda mrefu malalamiko yapo kwenye jamii.

"Hakuna shule iliyo huru kujifanyia mambo yake inavyotaka bila kujali taratibu zilizowekwa. Shule imekuwa vita kwa watoto wetu, Fikiria mtoto anatakiwa darasani saa 11 alfajiri hadi jioni, darasani hadi saa mbili usiku, ratiba hii ni mpaka Jumamosi, mwaka mzima.

"Mtoto hana ratiba ya kucheza, kukaa na ndugu zake, wazazi wake, anarudi nyumbani amechoka... saa 10 alfajiri ameamshwa. MAT ina wajibu wa kikatiba kuishauri serikali kuhusu mambo ya kiafya.

"Matron mmoja anatakiwa ahudumie watoto 20, bweni lina watoto 60 wa darasa la nne... watoto wanaingia darasani wana harufu, shule inayopokea 'boarding' lazima iwe na 'staff' wa kuhudumia watoto kwa vigezo vilivyowekwa," alibainisha Dk. Mwaibambe.

Alisema MAT itakapopata matokeo ya utafiti na kujua ukubwa wa tatizo, itakaa meza moja na Waziri wa Elimu na kutoa ushauri wa kiafya juu ya afya za watoto.

Januari mwaka huu, Nipashe ilichapicha ripoti kuhusu athari za wanafunzi kulazimishwa kukaa darasani kwa muda mrefu.

Septemba 10 mwaka huu, Nipashe pia ilichapisha ripoti kuhusu tatizo la wanafunzi kubeba mabegi mazito na madhara yake.

# Serikali yaja na hatua 6 kuzuia ukatili kijinsia

**Na Romana Mallya**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameagiza mambo sita yafanyike katika kukabiliana na ukatili wa kijinsia mojawapo ameelekeza madawati ya kushughulikia matatizo hayo yaanzishwe kuanzia shule za msingi hadi vyuo vikuu.

Majaliwa aliyasema hayo jana katika uzinduzi wa kampeni ya siku 16 za uanaharakati dhidi ya ukatili wa kijinsia uliokutanisha wadau mbalimbali ambapo pia alizindua mwongozo wa kuanzishwa kwa madawati hayo vyuo vikuu na vya kati.

Alisema asingependa kuona shule moja ina kuwa na walimu wa jinsia moja tu na kueleza kuwa kwa kufanya hivyo ni kuruhusu mianya ya kufanyika maovu na wanaofanyiwa washindwe kwa kukimbilia.

"Pili, vyuo vyote vya elimu ya juu na vya kati ambavyo bado havijaanzisha madawati haya navyo vikamilishe na itangazwe wazi ili wanachuo wote wajue" Agizo la tatu ni kwa Jeshi la Polisi, kwa kuwa mmeshaimarisha madawati, imarisheni itendaji kazi hususan kwenye maeneo yenye viashiria vingi vya ukatili wa kijinsia," alisema.

Alifafanua kuwa wanaposema shule za msingi na sekondari kuanzishwe madawati hawawezi kumpeleka mtu akakaa moja kwa moja wa jeshi la polisi lakini uwapo utaratibu wanaweza kupata taarifa za mara kwa mara, kwa mkuu wa shule kuanzisha idara na kumchagua mwalimu mwenye maadili ashughulie.

Agizo la nne alizitaja mamlaka za serikali za mitaa zikamilishe mradi wa kamati za ulinzi kwa wanawake na watoto kuanzia ngazi za chini ili wapate taarifa.

"Tano, programu za kuelimisha kuhusu madhara, vitendo vya ukatili wa kijinsia, ziendelezwe ili jamii ipate taarifa sahihi na zihusishe watu maarufu wanaokubalika na jamii husika wakiwamo viongozi wa dini, watu maarufu, wanasiasa, wazee wa mila," alisema.

Majaliwa alisema agizo lake la mwisho ni kwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, iendelee kujiimarisha na kushirikiana na sekta binafsi katika harakati za kukabiliana na matukio ya aina hiyo.

"Mfanye tathmini ya utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto na kuandaa mpango mpya; Kuimarisha mifumo ya utoaji wa taarifa za ukatili katika ngazi zote.

Mratibu wa Kitaifa wa kampeni hiyo, Anna Kulaya ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Afrika, alisema katika kipindi cha Januari mpaka Septemba mwaka huu, ripoti za Jeshi la Polisi zinaonyesha watoto 6,168 kati yao, wasichana ni 5,287 na wavulana 88, wamefanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia.

"Kati ya watoto hao, 3,524 walibakwa, 637 walilawitiwa, 1,887 walipata mimba na 130 walichomwa moto. Kinachosikitisha zaidi kati ya visa hivyo, watuhumiwa waliofikishwa mahakamani ni 3800 tu, kesi zilizofanyiwa upelelezi ni 2,368 na zilizotolewa hukumu ni 88 tu," alisema.

Naibu Waziri wa Afya, Mwanaidi Ali Khamis, alisema Wizara itaendelea kusimamia miongozo yote inayotolewa na wadau pamoja na washirika wa masuala ya jinsia ili kuhakikisha inapunguza kama siyo kutokomeza kabisa ukatili wa kijinsia.




# TAZARA yashtuka maiti kutupwa relini

**Na Thobias Mwanakatwe**

MAMLAKA ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA), imeeleza kushtuka kuwapo kwa matukio ya mara kwa mara ya maiti za watu waliouawa na watu wasiojulikana kutupwa relini ili ionekane wamegongwa na treni.

Kufuatia hali hiyo, TAZARA imeiomba serikali mkoani Songwe kufanya uchunguzi wa kina kubaini chanzo cha mauaji hayo ambayo yanazua maswali mengi kutoka kwa wananchi.

Mhandisi wa Ishara na Mawasiliano wa Wilaya ya Kitazara Mbeya, Betwel Kamugasha, alitoa ombi hilo jana kwenye kikao cha Bodi ya Barabara ya Mkoa kilichokuwa chini ya uenyekiti wa Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Omary Mgumba.

Kamugisha ambaye alimwakilisha Meneja wa TAZARA katika kikao hicho, alisema matukio hayo yamekuwa yakitokea mara kwa mara katika wilaya hiyo ya kitazara ya Mbeya inayohusisha mikoa ya Njombe, Mbeya na Songwe.

"Reli ya TAZARA inapita katika mikoa mitatu ya Njombe, Mbeya na Songwe kwa upande wa Wilaya ya Mbeya kitazara, kwa hiyo matukio ya maiti kutupwa relini mara kwa mara huwa yanatokea maeneo tofauti tofauti katika mikoa hii," alisema.

Aliongeza: "Kuna muda mwingine mnakuta maiti ya mtu kagongwa na treni, lakini kuna maiti nyingine zinaonekana mtu aliuawa na watu wasiojulikana na kuja kuitupa relini ili ionekane aligongwa na treni...sasa nimewasilisha changamoto hii ili mkuu wa mkoa naye aweze kuiwasilisha kwenye kamati yake ya ulinzi na usalama ili waone namna gani wanaweza kufanya uchunguzi matukio hayo yaweze kukoma," alifafanua Kamugisha.

Aidha, Kamugisha alisema changamoto nyingine inayoikumba mamlaka hiyo ni hujuma ambapo watu wamekuwa wakiharibu miundombinu kwa kung'oa mataruma ya reli na kwenda kuviuza kama vyuma chakavu.

Alisema uharibifu huo wa miundombinu umekuwa ukijitokeza mara kwa mara, hivyo kuhatarisha usalama wa treni na kuiomba serikali kwa kushirikiana na TAZARA kufanya uchunguzi kubaini wanaofanya hujuma hizo kuchukuliwa hatua.

Akijibu maombi hayo, Mkuu wa Mkoa Songwe, Mgumba, alisema wamelipokea kama serikali kwa kutumia vyombo vyake vya usalama litafanyiwa kazi.

Pia alisema serikali na wananchi kwa ujumla wana jukumu la msingi kuilinda reli ya TAZARA kwa maslahi mapana ya uchumi wa Taifa.




Waziri wa Mambo ya Ndani, George Simbachawene (wa nne kulia), akikata utepe kuzindua sehemu maalum ya kusimama pikipiki (bodaboda), wakati taa nyekundu inapowaka barabarani, jijini Arusha, jana. Kulia kwake ni Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Khamis Hamza Chilo na wapili kushoto ni Mwakilishi wa Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Ujenzi), Mhandisi Kashinde Musa. **PICHA: WMNN**

# WB yakunwa wanaopata ujauzito kurudi shuleni

**Na Waandishi Wetu**

BENKI ya Dunia (WB) imepongeza uamuzi wa Tanzania kuruhusu wanafunzi waliokatisha masomo kwa sababu mbalimbali, ikiwamo ujauzito, kurejea masomoni katika mfumo rasmi baada ya miaka miwili.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa umma juzi na WB Washington DC, Marekani, uamuzi huo ni mzuri kwa kuwa unasaidia kuwawezesha wasichana wadogo walioacha masomo yao kupata elimu bora kwa utaratibu rasmi.

"Zaidi ya wasichana 120,000 wanaacha masomo kila mwaka Tanzania, 6,500 kwa sababu wana mimba," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

WB ilibainisha inasaidia sera zinazowawezesha elimu kwa wasichana kwa kuhakikisha wanafunzi wote wanakaa shuleni.

WB ilisema itashirikiana na serikali kuhakikisha kunakuwa na mwongozo wa kuwezesha wasichana waliopata mimba na mama wadogo kuendelea na masomo.

**JICHO LA LHRC**

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, aliiambia Nipashe jana kuwa ili kuwe na utekelezaji wa suala hilo kwa asilimia 100, kuna haja litungiwe sheria.

Alisema suala hilo halitakuwa la kudumu kama halitawekewa sheria maalum, huku akiwataka wanafunzi husika kuitumia fursa hiyo ipasavyo ili kuyafikia malengo yao.

"Tunaipongeza serikali kwa hatua iliyofikia lakini tunaendelea kutoa wito kwa wadau wa sera waweke maboresho na sera itakayotumiwa na waziri yoyote dhidi ya suala hilo ili liwe la kudumu, pia ninatoa wito kwa walimu shuleni waweze kuwasimamia vizuri wanafunzi," alishauri Anna.

Mkurugenzi wa Utetezi na Maboresho kutoka LHRC, Fulgence Masawa, aliipongeza serikali kwa kufikia hatua hiyo, huku akidai kuwa kilichofanyika kina faida kwa mtoto wa kike. Alisema siku chache zilizopita walipeleka shauri mahakamani kwa ajili ya kudai haki ili kumsaidia mtoto wa kike aliyepatwa na kadhia ya kuacha shule.

Aliipongeza serikali kwa kuonyesha utayari wa kukubali mapendekezo yao yanayomwekea mazingira mazuri mwanafunzi.

# Serikali, wadau waketi kusaka fedha za miradi

**Na Romana Mallya**

SERIKALI na washirika wa maendeleo wamekutana kujadili mambo mbalimbali ambayo yataingizwa kwenye sera, miongozo, bajeti ijayo na mipango ya taasisi ili kuwezesha kupata fedha za kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mwenyekiti wa mazungumzo hayo ambaye ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam katika mkutano wa majadiliano ya kimkakati kati ya pande hizo mbili.

Tutuba alisema kikao hicho kimeandikwa kwenye mkakati waliokubaliana ambao kwa pamoja waliusaini kutekeleza miradi.

"Kikao hiki ni cha siku mbili, tumeanza na makatibu wakuu na wakuu wa mashirika ya kimataifa na wadau wa maendeleo, kesho (leo) kitahusisha mawaziri, mabalozi na taasisi za kimataifa. Kwa mara ya kwanza kikao hiki kimeshirikisha asasi za kiraia na tumewaalika sekta binafsi kwa sababu wana mchango mkubwa katika miradi mbalimbali ya maendeleo," alisema. Tutuba alisema Juni wakati wanazindua Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, walialika wadau wote kushiriki kwenye ujenzi wa uchumi imara.

"Sasa ndichoo kipindi cha kuandaa mwongozo na mipango ya bajeti ya serikali ya mwaka 2022/23, tunatarajia mambo tutakayojadili hapa yatasaidia misingi ya kuandaa sera, tutakwenda kuandaa mipango halisi ya kila wizara, mikoa na halmashauri ambazo zitatokana na majadiliano haya," alisema.

Kwa mujibu wa Tutuba, katika mawasilisho wadau wataainisha mambo yaliyojitokeza, yakiwamo matatizo na mapendekezo yao ambayo serikali itaangalia namna ya kuyaingiza kwenye bajeti na mipango ya mwakani.

"Kutakuwa na mada mbalimbali na mojawapo inaonyesha mpango wa maendeleo wa miaka mitano ili tuwafahamishe wadau wetu wa maendeleo masuala gani ya kipaumbele ili watushauri, tutapata fursa ya kujadiliana nao ili watupatie fedha kwenye maeneo wanaona watashiriki," alisema.

"Tunakubaliana na sekta binafsi kwenye maeneo ambayo wanataka kushirikiana na serikali tupo tayari tumwalika yeyote mwenye fedha zake, utaalam au kitu ambacho kitaongeza kasi ya miradi ya maendeleo aje, sera zipo wazi. Tunatarajia karibu asilimia 30 ya miradi itatekelezwa kwa ubia kati ya sekta ya umma na binafsi," alisema.

Alitoa rai kwa sekta binafsi iendelee kushiriki katika ukuzaji wa uchumi na miradi ya ngazi mbalimbali kuanzia midogo hadi mikubwa.

Mwenyekiti mwenza ambaye anawakilisha washirika wa maendeleo, Zlatan Milisic, aliipongeza serikali kwa hatua iliyofikia juzi ya kuwarejesha mashuleni watoto waliopata ujauzito. Alisema hatua kubwa zaidi ambazo serikali inapaswa kuchukua ni kutazama mikakati yake kwenye suala la kijinsia na bajeti zake kwani ni muhimu. Mkurugenzi wa Sera na Utafiti kutoka Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Andrew Mahiga, alisema wito wa sekta binafsi ni kuingia ubia kuchangia mpango huo wa maendeleo.

Kuhusu sekta binafsi kualikwa kwenye kikao hicho, Mahiga alisema tangu awamu ya sita iingie madarakani wamepata fursa mbalimbali ikiwamo kukutana na Rais Samia Suluhu Hassan, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na mawaziri.

# MATANGAZO

EAST AFRICAN
**CRUDE OIL PIPELINE**

## OMBI LA KUONESHA NIA UTENEGENEZAJI NA USAMBAZAJI WA MADIRISHA
## KUMBUKUMBU: 0010007285

Kampuni ya Kimataifa ya Mafuta na Gesi ya TotalEnergies East Africa Midstream B.V, inaalika taasisi zenye weledi na uzoefu kuonesha nia ya kutoa huduma ya utengenezaji na usambazaji wa madirisha katika Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini ya ardhi litakalovuka mipaka ya nchi mbili na litakalosafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika masoko ya Kimataifa. Bomba hili litaanzia Kabaale katika wilaya ya Hoima nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania. Urefu wa Bomba ni kilomita 1,443, kati ya hizo, kilomita 1,147 zitakuwa Tanzania, ambapo bomba hilo litapita kwenye mikoa minane (8) ambayo ni Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara, na Tanga; bomba la mafuta pia litapita kwenye Halmashauri za Wilaya 27 na vijiji 231.

**MAELEZO MAFUPI KUHUSU MAWANDA YA HUDUMA:**

EACOP inahitaji huduma za mtengenezaji mwenye uzoefu na mwenye sifa nzuri kutoa huduma za Utengenezaji na Usambazaji wa Madirisha aina ya Aluminium, kulingana na viwango, vipimo na maelezo yaliyotajwa hapa chini:

**VIWANGO:**

Nyenzo, uzalishaji na uunganishaji wa madirisha ya Aluminium utazingatia viwango BS 4873:2009 – Muongzo wa Madirisha ya Aluminium. Vipimo, pamoja na marekebisho yake ya hivi karibuni, isipokuwa ikiwa imeainishwa vinginevyo.

**VIPIMO:**

Dirisha lenye unene wa 80 x 27 x 1mm Aluminium na yenye ukubwa wa jumla wa 1200 x1200mm juu, inayojumuisha cha mm 5 chenye chandarua chenye nyuzinyuzi 0.25 x 1mm, chuma cha grill chenye ukubwa 25 x 4mm (100x100) uliopakwa rangi na waya wa kahawa. Pamoja na vifungio na na vifaa vyovyote vinavyohusika.

Dirisha lenye unene wa 80 x 27 x 1mm Aluminium na yenye ukubwa wa jumla wa 900 x1200mm juu, inayojumuisha cha mm 5 chenye chandarua chenye nyuzinyuzi 0.25 x 1mm, chuma cha grill chenye ukubwa 25 x 4mm (100x100) uliopakwa rangi na waya wa kahawa. Pamoja na vifungio na na vifaa vyovyote vinavyohusika.

**VIGEZO MUHIMU:**

MSAMBAZAJI atakuwa na uwezo wa kiwango cha chini cha uzalishaji cha madirisha 150 kwa mwezi ili kukidhi kiwango kitakachohitajika na KAMPUNI. KAMPUNI inategemea kuwa na uhitaji wa angalau madirisha 1200 kwa jumla, kwa kiwango kilichoainishwa hapo juu cha madirisha 150 kwa mwezi.

- KAMPUNI inahifadhi haki ya kuthibitisha utengenezaji wa madirisha katika eneo la Mtengenezaji kulingana na mfumo wa usimamizi wa ubora sawasawa na viwango vilivyoainishwa.
- Hakuna nyenzo au viambatisho vitatumika katika utengenezaji hadi kibali cha awali cha matumizi yake kitolewe na KAMPUNI; wala mabadiliko yoyote katika asili, ubora, aina, na aina, chanzo cha usambazaji hakitafanywa bila ruhusa ya KAMPUNI.
- Kwa ombi, nyaraka za ubora wa bidhaa zinazotolewa zinapaswa kuwasilishwa na mtengenezaji kupitia vyeti vya kufanya kazi kulingana na viwango vinavyotumika. Rekodi zote za matokeo ya vipimo vya ubora zitahifadhiwa na mtengenezaji kwa marejesho yajayo.
- Kabla na baada ya kutoa zabuni kwa Mtengenezaji, KAMPUNI ina haki ya kukagua uwezo wa upimaji na kushuhudia majaribio yaliyofanywa katika kituo cha Maabara cha Mtengenezaji kutathmini ubora wa bidhaa kulingana na viwango vinavyotumika.
- KAMPUNI itateua mwakilishi kushuhudia majaribio yote yaliyofanywa katika kituo cha maabara cha Mtengenezaji na mwakilishi atawasilisha matokeo yote ya mkandarasi/mzabuni husika & KAMPUNI kwa kujitegemea. KAMPUNI ina haki ya kuidhinisha Bidhaa kulingana na ripoti za majaribio ya ubora kabla ya kupelekwa kwenye eneo la ujenzi.
- Madirisha na maunzi yake yote yatakuja na dhamana ya vifaa na utengenezaji kwa muda wa miezi 12 tangu tarehe ya kukabidhi.

**VIGEZO MUHIMU VYA KUZINGATIA:**

Taasisi zitakazoonesha nia zinaalikwa kuambatanisha maombi yao pamoja na taarifa zifuatazo:

- Uzoefu, utendaji, na uwezo katika kutekeleza kazi zilizoainishwa chini ya upeo wa kazi, kwa kiwango kikubwa nchini Tanzania, kwa kufuata viwango vya kitaifa na kimataifa (ikiwa ni pamoja na Viwango vya Shirika la Fedha la Kimataifa (IFC), na uzoefu wa angalau miaka 15 katika utendaji wa huduma kama hizo ndani ya Tanzania au Kimataifa.
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na cheti cha uthibitisho wa kulipa kodi kwa mwaka wa fedha uliopita.

**Maelezo mafupi kuhusu uzoefu na uwezo wa:**

- Utekelezaji wa programu za aina hiyo kwa viwango vya fedha vya kimataifa kwa ajili ya miradi mikubwa ya miundombinu nchini Tanzania.
- Kusimamia miradi mikubwa na wakandarasi washirika.
- kufanya kazi kwa kushirikiana na serikali za mitaa na sekta binafsi.
- Wafanyakazi waliopendekezwa kufanya kazi kwenye Mradi huu na ujuzi na uzoefu wao katika kutekeleza programu za aina hii.
- Inashauriwa, mwonyesha nia atume maombi ya kusajiliwa na kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia ya kutekeleza shughuli za progamu.
- Kuzingatia Kanuni za maudhui ya ndani, 2017 na ufafanuzi wa Kampuni ya Ndani.

**Mawanda haya yanaweza kugawanywa kimkoa au kiutalaam na KAMPUNI inaruhusu Wazabuni kuwasilisha pendekezo kwa ajili ya kipengele kimoja, kadhaa au vyote.**

---

Taasisi zenye nia ya kuleta maombi na ambazo zina uwezo na rasilimali za kutekeleza shughuli au kazi zilizoorodheshwa hapo juu zinapaswa kueleza nia yao pamoja na kuambatanisha pamoja na nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwa **eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa wa barua pepe 20 Mb) saa au kabla ya saa **11** jioni za Afrika Mashariki (EAT) tarehe **08 Disemba 2021.** Kichwa cha Habari cha barua pepe ni **0010007285.**

---

**Muhimu:** Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na taasisi zitakazoonyesha nia iii kutengeneza orodha ya taasisi za awali zenye vigezo vinavyotakiwa. Taasisi zitakazokidhi vigezo iu ndiyo zitapokea na kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA) pamoja na mwaliko wa kuwasilisha zabuni katika kuendeleza mchakato wa zabuni. Maelezo yote ya kuonyesha nia yanapaswa kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza.

EAST AFRICAN
**CRUDE OIL PIPELINE**

## OMBI LA KUONESHA NIA USAMBAZAJI WA MAJOPO YA NISHATI YA JUA
## KUMBUKUMBU: 0010007283

Kampuni ya Kimataifa ya Mafuta na Gesi ya TotalEnergies East Africa Midstream B.V, inaalika taasisi zenye weledi na uzoefu kuonesha nia ya kutoa huduma ya usambazaji wa majopo ya nishati ya jua katika Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini ya ardhi litakalovuka mipaka ya nchi mbili na litakalosafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika masoko ya Kimataifa. Bomba hili litaanzia Kabaale katika wilaya ya Hoima nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania. Urefu wa Bomba ni kilomita 1,443, kati ya hizo, kilomita 1,147 zitakuwa Tanzania, ambapo bomba hilo litapita kwenye mikoa minane (8) ambayo ni Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara, na Tanga; bomba la mafuta pia litapita kwenye Halmashauri za Wilaya 27 na vijiji 231

**MAELEZO MAFUPI KUHUSU MAWANDA YA HUDUMA:**

EACOP inahitaji huduma za mtengenezaji mwenye uzoefu na mwenye sifa nzuri kutoa huduma za Usambazaji wa Majopo ya Nishati ya Jua (Sola) na vifaa vyake kulingana na viwango, vipimo na maelezo yaliyotajwa hapa chini:

**VIWANGO:**

Nyenzo, uzalishaji na mkusanyiko wa vifaa vya Umeme wa Jua vitazingatia viwango vifuatavyo:

**VYETI VYA MFUMO WA USIMAMIZI:**

ISO 9001:2015 / Mfumo wa usimamizi wa ubora; ISO 14001:2015 / Viwango vya mfumo wa usimamizi wa mazingira; ISO 45001: 2018 / Viwango vya kimataifa vya afya na usalama kazini, pamoja na marekebisho yake ya hivi punde, isipokuwa kama itabainishwa vinginevyo.

**VYETI VYA BIDHAA:**

IEC 61215 / IEC 61730 / CE / MCS / IN METRO; CEC (US California) / FSEC (US Florida); UL 61730 / IEC 61701 / IEC 62716 ; ISO 9001: kuthibitishwa 2015; ISO 14001: Udhibitisho wa 2015 unaoashiria ufahamu wa mazingira; OHSAS 18001: 2007 iliyoidhinishwa, na marekebisho yake ya hivi punde, isipokuwa ikiwa imebainishwa vinginevyo.

**VIBALI VYA BIDHAA**

Iwe inalingana na IEC 60896; IEC 61427; IS 15549 & IS 16220 Inalingana na JIS C 8702; IEC 62109-1/-2, IEC 62116, EN 61000-6-1/-2/-3/-4, pamoja na marekebisho yake ya hivi karibuni, isipokuwa ikiwa imebainishwa vinginevyo.

**JOPO LA NISHATIYA JUA ITAJUMUISHA VIFUATAVYO:**

- Jopo la nishati ya jua yenye uwezo wa Wati 400.
- Kibadilishaji kigeuzi kinacholingana chenye wigo mpana wa volteji
- 12V – 200 AH betri.
- Chaja controla.

**VIGEZO MUHIMU:**

- MSAMBAZAJI atakuwa na uwezo wa kiwango cha chini cha usambazaji wa Majopo ya nishati ya jua (Sola) 30 na vifaa vyake kwa mwezi ili kukidhi kiwango kitakachohitajika na KAMPUNI. KAMPUNI inategemea kuwa na uhitaji wa angalau majopo ya nishati ya jua (Sola) 220 na vifaa vyake kwa jumla, kwa kiwango kilichoainishwa hapo juu cha Jopo za nishati ya jua (Sola) 30 na vifaa vyake k w a mwezi.
- Hakuna nyenzo au viambatisho vitatumika katika utengenezaji hadi kibali cha awali cha matumizi yake kitolewe na KAMPUNI; wala mabadiliko yoyote katika asili, ubora, aina, na chanzo cha usambazaji hakitafanywa bila ruhusa ya KAMPUNI.
- Kwa ombi, nyaraka za ubora wa bidhaa zinazotolewa zinapaswa kuwasilishwa na mtengenezaji kupitia vyeti vya kufanya kazi kulingana na viwango vinavyotumika. Rekodi zote za matokeo ya vipimo vya ubora zitahifadhiwa na mtengenezaji kwa marejesho yajayo.
- Kabla na baada ya kutoa zabuni kwa Mtengenezaji, KAMPUNI ina haki ya kukagua uwezo wa upimaji na kushuhudia majaribio yaliyofanywa katika kituo cha Maabara cha Mtengenezaji na kutathmini ubora wa bidhaa kulingana na viwango vinavyotumika.
- KAMPUNI itateua mwakilishi kushuhudia majaribio yote yaliyofanywa katika kituo cha maabara cha Mtengenezaji na mwakilishi atawasilisha matokeo yote ya mkandarasi/mzabuni husika & KAMPUNI kwa kujitegemea. KAMPUNI ina haki ya kuidhinisha Bidhaa kulingana na ripoti za majaribio ya ubora kabla ya kupelekwa kwenye eneo la ujenzi.
- Jopo la nishati ya jua na maunzi yake yote yatakuja na dhamana ya vifaa na utengenezaji kwa muda wa miezi 12 tangu tarehe ya kukabidhi.

**VIGEZO MUHIMU VYA KUZINGATIA:**

Taasisi zitakazoonesha nia zinaalikwa kuambatanisha maombi yao pamoja na taarifa zifuatazo:

- Uzoefu, utendaji, na uwezo katika kutekeleza kazi zilizoainishwa chini ya upeo wa kazi, kwa kiwango kikubwa nchini Tanzania, kwa kufuata viwango vya kitaifa na kimataifa (ikiwa ni pamoja na Viwango vya Shirika la Fedha la Kimataifa (IFC), na uzoefu wa angalau miaka 10 katika utendaji wa huduma kama hizo ndani ya Tanzania au kimataifa
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na cheti cha uthibitisho wa kulipa kodi kwa mwaka wa fedha uliopita.
- Maelezo mafupi kuhusu uzoefu na uwezo wa:
- Utekelezaji wa programu za aina hiyo kwa viwango vya fedha vya kimataifa kwa ajili ya miradi mikubwa ya miundombinu nchini Tanzania.
- Kusimamia miradi mikubwa na wakandarasi washirika.
- kufanya kazi kwa kushirikiana na serikali za mitaa na sekta binafsi.
- Wafanyakazi waliopendekezwa kufanya kazi kwenye Mradi huu na ujuzi na uzoefu wao katika kutekeleza programu za aina hii.
- Inashauriwa, mwonyesha nia atume maombi ya kusajiliwa na kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia ya kutekeleza shughuli za progamu.
- Kuzingatia Kanuni za maudhui ya ndani, 2017 na ufafanuzi wa Kampuni ya Ndani

**Mawanda haya yanaweza kugawanywa kimkoa au kiutalaam na KAMPUNI inaruhusu Wazabuni kuwasilisha pendekezo kwa ajili ya kipengele kimoja, kadhaa au vyote.**

---

Taasisi zenye nia ya kuleta maombi na ambazo zina uwezo na rasilimali za kutekeleza shughuli au kazi zilizoorodheshwa hapo juu zinapaswa kueleza nia yao pamoja na kuambatanisha pamoja na nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwa **eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa wa barua pepe 20 Mb) saa au kabla ya saa **11** jioni za Afrika Mashariki (EAT) tarehe **08 Disemba 2021.** Kichwa cha Habari cha barua pepe ni **0010007283.**

---

**Muhimu:** Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na taasisi zitakazoonyesha nia iii kutengeneza orodha ya taasisi za awali zenye vigezo vinavyotakiwa. Taasisi zitakazokidhi vigezo iu ndiyo zitapokea na kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA) pamoja na mwaliko wa kuwasilisha zabuni katika kuendeleza mchakato wa zabuni. Maelezo yote ya kuonyesha nia yanapaswa kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Bravo serikali, lakini bado kuna maswali

**SERIKALI** imetoa Waraka wa Elimu namba 2 mwaka 2021 kuhusu urejeshwaji shuleni wa wanafunzi waliokatiza masomo katika elimu ya msingi na sekondari kwa sababu mbalimbali.

Wanafunzi wanaohusika ni waliokatiza masomo kutokana na sababu mbalimbali kama utoro, utovu wa nidhani na kupata ujauzito, pia baadhi ya wanafunzi hushindwa kuhudhuria masomo kwa muda mrefu kutokana na changamoto za kifamilia au wazazi kuhama maeneo bila kufuata taratibu za uhamisho wa watoto wao.

Aidha, utekelezaji wa waraka huo umeanza Novemba 24, mwaka huu, na umeangalia maeneo matano ambayo ni wanafunzi watakaokatiza masomo kutokana na ujauzito au utoro wataruhusiwa kurudi shuleni ndani ya miaka miwili tangu walipokatiza masomo.

Wakuu wa shule/walimu wakuu wahakikishe wanafunzi waliokatiza masomo na kurudi shuleni wanapata huduma za ushauri na unasihi ili kuwajenga kisaikolojia sambamba na wanafunzi wengine waliopo shuleni. Pia, wahakikishe mwanafunzi aliyekatiza masomo anarejea mwanzoni mwa mwaka wa masomo katika darasa alilokuwa anasoma. Aidha, walimu wahakikishe mchakato wa ujifunzaji na ufundishaji unafanyika katika mazingira bora kwa wanafunzi wote.

Pia, viongozi wa elimu katika ngazi zote wafuatilie na kutathmini utekelezaji wa waraka huo, huku mipaka ya waraka ikitajwa kuwa hautahusu wanafunzi waliofukuzwa shule kutokana na makosa yenye mawelekeo wa jina au mwenendo unaohatarisha amani shuleni, na kwamba watakaothibitika kutenda makosa hayo na kufukuzwa shule wanashauriwa kuendelea na masomo kupitia elimu nje ya mfumo rasmi.Uamuzi huu umepokelewa kwa shangwe kubwa na watetezi wa haki za wasichana na watoto kwa kuwa wapo ambao walipata ujauzito kwa kubakwa na siyo kwamba walijiingiza kwenye mahusiano ya kimapenzi wakiwa masomoni.

Tunaipongeza serikali kwa uamuzi huu kwa kuwa sasa unakwenda kuongeza idadi ya wasichana ambao ndoto zao zingekufa, lakini sasa tutakuwa na watu walioelimika watakaolea watoto wao vyema na kutoa mchango kwenye maendeleo ya familia zao na taifa kwa ujumla. Wengi walijikuta wakikatisha ndoto zao na kushindwa kujiendeleza na matokeo yake kuendelea kupunguza idadi ya wasichana wasomi na wanawake wa baadaye ambao watatoa mchango kwa taifa lao. Wapo wanaoesma uamuzi huo utawafanya wanafunzi wanaojihusisha na mapenzi kuwa ni jambo la kawaida, kwa kuwa hakuna adhabu ya kuwafanya wasiendelee na masomo, bali baadaye watarudi na huenda itachochea ongezeko la mimba za utotoni.


Maswali yaliyopo kwa watu ni Je? ndiyo ruksa mabinti wa umri mdogo kushiriki kwenye kujamiiana, na je, itakuwa kwa mimba moja na mtoto mmoja tu au anaweza kufululiza kupata ujauzito, kujifungua baada ya miaka miwili anarudi shule, mwakani anabeba mimba nyingine na nyingine, pia ataruhusiwa kwenda na mwanaye shuleni na kama kuna vituo vya watoto wadogo shuleni.

Kuna umuhimu maswali haya yakajibiwa na serikali ili kurahisisha utekeleza wa waraka huu na kuwafanya wasome na kufikia malengo yao, ili shuleni pasigeuke kuwa mahali pa kuwaumiza tena.


Lakini ni namna watoto hawa hawa watarudi kwenye shule zile zile ambazo wenzao walijua kuwa walipata mimba, lakini hawajui walipata kwa kukubali, kurubuniwa au kubakwa na huenda kutakuwa na unyanyapaa au kuwaumiza kisaikolojia kuwa tayari wameshaondoka kwenye usichama na sasa ni mama.

Waraka umetaka walimu kutoa ushauri nasaha kwa wanafunzi hawa, jambo ambalo ni muhimu kama litatekelezwa kikamilifu, ili kuwajengea ujasiri wa kukubali hali halisi na kurudi kwenye ndoto zao. Kadhalika, ni muhimu jamii inayowazunguka nayo ikawa na uelewa wa kutosha utakaosaidia wanafunzi hao kusoma kama wengine badala ya kunyooshewa vidole. Tunaamini waraka huu utatekelezwa ipasavyo, pia ni muhimu ukasambazwa kila mahali ili kuwe na uelewa kwa jamii na wazazi ili waruhusu watoto wao kuendelea na masomo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Hii ndio picha ya ukatili kijinsia ulivyo, upana na undani wake

Na Yasmine Protace

**HIVI** sasa katika kuelekea Maadhimisho ya Siku 6 za Kupinga Ukatili wa Kijinsa, unaofanyika kila mwaka kati ya Novemba 25 hadi Desemba 10, kuna mengi yanaendelea kila kona.

Ni jana tu Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alikuwa na jumuiya ya wasomi akiwaachia miongozo kadhaa namna ya kukabili adha za kijinsia.

Siku moja kabla kwa maana ya juzi tulimsikia Waziri Prof. Joyce Ndalichako, mtaalamu wa elimu na aliyepewa dhamana kitaifa kuwajibikia elimu, alitangaza jipya katika historia ya nchi, kwamba waliopata ujauzito wanapewa fursa yao kurejea shule waendelee na masomo.

Najua limeshazungumzwa sana, lakini bado ni wajibu wa kila mmoja wetu kumkumbusha mwenzake, haki za kijinsia namna ya kuzitetea.

Ukweli ni kwamba ukatili wa kijinsia, umekuwa ukifanywa na baadhi ya watu, huku kuna kundi la wanaofanyiwa ukatili wanashindwa kutoa ushirikiano unaowezesha wakosaji wachukuliwe hatua.

Huu ukatili wa kijinsia upo wa aina mbalimbali, ambao umekuwa ukiendelea kufanywa katika makundi kama ya wanawake, watoto wa kike, wanaume kufanyiwa ukatili pia hata upo wa kiuchumi; ni mustakabali mpana.

Wakati tunaendelea na maadhimisho haya wiki mbili na siku mbili kupinga ukatili, baadhi ya wanaharakati wanaendesha semina za jinsia na maendeleo kutoka pande zaidi, ikiwano inayoratibiwa na asasi kama ya THNP na wanaotoa maoni yao kwa nyakati tofauti, nini kifanyike ili kutokomeza matukio hayo.

Bishagazi Suleimani, ni mshiriki mafunzo ya aina hiyo, anayesema ili kutokomeza matukio hayo, ni muhimu jamii ikawa na nguvu ya pamoja katika kutokomeza ukatili wa namna hiyo.

Anasema, pale inapowezekana, serikali inapaswa kuanza kutoa elimu ya matukio hayo kwa watoto wadogo wa shule za msingi, kuanzia darasa la pili na kuendelea hadi wapatiwe elimu hiyo waweze kuelewa ukatili.

" Watoto hao ndio asilimia kubwa wamekuwa wakifanyiwa matukio ya ukatili, ukifuatilia utasikia ukatili kafanyiwa na baba wa kufikia, baba mdogo au ndugu yao wa karibu," anasema.

Anaongeza kuwa, kungefanyika mabadiliko katika elimu, mtoto akifanya mtihani wa darasa la nne au mtihani wa kidato pili, wasikae nyumbani kusubiri matokeo, kinachotakiwa waendelee na masomo.

Anafafanua kwamba kukaa kwake nyumbani kunachangia mtoto kujiingiza katika michezo isiyofaa.

Pia, Zahara Omary anasema, ili kutokomeza ukatili inatakiwa nguvu ya pamoja iwapo, katika namna nyingi.

Zahara anataja kuyafikia malengo ya kutokomeza ukatili, inatakiwa kusiwapo usiri na nguvu ya pamoja ndio ichukue nafasi kwa kuchukua hatua dhidi ya wanaofanya ukatili huo.

Hapo anazungumzia mkasa wa kilichotokea katika eneo mojawapo katika Kata ya Ukonga jijini Dar es Salaam, anasema kuna mwanafunzi wa shule ya msingi alikuwa akifanyiwa vitendo vya kikatili na baba wa kambo.

Anafafanua kuwa, mtoto huyo alishindwa kutoa taarifa kwa mtu yoyote, akihofia hatima ya usalama wake. Mtoto huyo aligunduliwa shuleni, baada ya kuonekana hayupo vizuri kiafya.

"Baada ya mtoto kugundulika hayupo vizuri aliletwa katika ofisi zetu za jamii yulipo muhoji alisema baba wakufikia amekuwa akimdhalilisha na alimwambia akitoa siri hiyo atamuuwa,"anasimulia mdai huyo.

ZAnaongeza kuwa mtoto huyo wamemtafutia pa kuishi kutokana na hapa kwao kukataa kwenda.

Joyce Mkina, kutoka TGNP Mtandao anatoa siku maalum za maadhimsho, akitaja siku za kupinga ukatili wa kijinsia kukiambatana na matukio mbalimbali, akitoa mfano Novemba 25 ni siku ya kupinga ukatili wa kijinsia.

Anasema Novemba 29 ni siku ya kimataifa ya utetetezi wa haki za wanawake, huku Desemba Mosi ni siku ya Ukimwi duniani, Desemba 5 ni mahsusi Siku ya kujitolea Duniani, huku Desemba 10 ni Siku ya Kimataifa ya Haki za Binadamu.

# MATANGAZO

EAST AFRICAN
CRUDE OIL
PIPELINE

## OMBI LA KUONESHA NIA UTENGENEZAJI NA USAMBAZAJI WA MABATI
## KUMBUKUMBU: 0010007287

Kampuni ya Kimataifa ya Mafuta na Gesi ya TotalEnergies East Africa Midstream B.V, inaalika taasisi zenye weledi na uzoefu kuonesha nia ya utengenezaji na usambazaji wa mabati katika Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini ya ardhi litakalovuka mipaka ya nchi mbili na litakalosafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika masoko ya Kimataifa. Bomba hili litaanzia Kabaale katika wilaya ya Hoima nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania. Urefu wa Bomba ni kilomita 1,443, kati ya hizo, kilomita 1,147 zitakuwa Tanzania, ambapo bomba hilo litapita kwenye mikoa minane (8) ambayo ni Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara, na Tanga; bomba la mafuta pia litapita kwenye Halmashauri za Wilaya 27 na vijiji 231.

**MAELEZO MAFUPI KUHUSU MAWANDA YA HUDUMA**

EACOP inahitaji huduma za mtengenezaji mwenye uzoefu na mwenye sifa nzuri kutoa huduma za Utengenezaji na Usambazaji wa Profaili za Mabati kulingana na viwango, vipimo na maelezo yaliyotajwa hapa chini:

**VIWANGO:**

Nyenzo, uzalishaji na mkusanyiko wa mabati itazingatia EAS 468; 2019 Kiwango cha Afrika Mashariki cha mabati yaliyopakwa rangi ya awali - Maelezo, pamoja na marekebisho yake ya hivi punde, isipokuwa ikiwa imebainishwa vinginevyo.

**TAARIFA ZA JUMLA ZA BATI/PAA**

- Nguvu ya Mavuno ya Chuma: 550MPa
- Kiwango cha Mipako ya Aluminium-Zinki kwenye chuma: AZ85
- Uzito wa rangi: Mikroni 19
- Unene wa geji ya bati: 28G (0.32mm)
- Wasifu: Ubavu wa Kisanduku Uliogeuzwa
- Upana wa bati: 800mm - 1100 mm

**VIGEZO MUHIMU:**

- KAMPUNI inahifadhi haki ya kuthibitisha uundaji wa mabati katika kiwanda cha Mtengenezaji kulingana na mfumo wa usimamizi wa ubora kulingana na ISO 9001:2015.
- MSAMBAZAJI atatakiwa kuwa na uwezo wa kiwango cha chini cha uzalishaji wa mabati cha uzalishaji cha mita za mraba 2100 za mabati kwa mwezi ili kukidhi kalenda ya matukio ya KAMPUNI. KAMPUNI inategemea kuwa na uhitaji wa wa kima cha chini cha jumla ya mita za mraba 17,000 za mabati, kwa kiwango kilichoainishwa hapo juu cha mita za mraba 2100 kwa mwezi.
- KAMPUNI inahifadhi haki ya kuthibitisha utengenezaji wa mabati ambazo zitakazoidhinishwa katika eneo la Mtengenezaji/kiwanda kulingana na mfumo wa usimamizi wa ubora sawasawa na viwango vilivyoainishwa.
- Hakuna nyenzo au viambatisho vitatumika katika utengenezaji wa mabati hadi kibali cha awali cha matumizi yake kitolewe na KAMPUNI; wala mabadiliko yoyote katika asili, ubora, aina, na chanzo cha usambazaji hakitafanywa bila ruhusa ya KAMPUNI.
- Kwa ombi, nyaraka za ubora wa bidhaa zinazotolewa zinapaswa kuwasilishwa na mtengenezaji kupitia vyeti vya kufanya kazi kulingana na viwango vinavyotumika. Rekodi zote za matokeo ya vipimo vya ubora zitahifadhiwa na mtengenezaji kwa marejesho yajayo.
- Kabla na baada ya kutoa zabuni kwa Mtengenezaji, KAMPUNI ina haki ya kukagua uwezo wa upimaji na kushuhudia majaribio yaliyofanywa katika kituo cha Maabara cha Mtengenezaji kutathmini ubora wa bidhaa kulingana na viwango vinavyotumika.
- KAMPUNI itateua mwakilishi kushuhudia majaribio yote yaliyofanywa katika kituo cha maabara cha Mtengenezaji na mwakilishi atawasilisha matokeo yote ya mkandarasi/mzabuni husika & KAMPUNI kwa kujitegemea. KAMPUNI ina haki ya kuidhinisha Bidhaa kulingana na ripoti za majaribio ya ubora kabla ya kupelekwa kwenye eneo la ujenzi.
- Mabati pamoja na maunzi yake yote yatakuja na dhamana ya vifaa na utengenezaji kwa muda wa miezi 12 tangu tarehe ya kukabidhi.

**VIGEZO MUHIMU VYA KUZINGATIA:**

Taasisi zitakazoonesha nia zinaalikwa kuambatanisha maombi yao pamoja na taarifa zifuatazo:

- Uzoefu, utendaji, na uwezo katika kutekeleza kazi zilizoainishwa chini ya upeo wa kazi, kwa kiwango kikubwa nchini Tanzania, kwa kufuata viwango vya kitaifa na kimataifa (ikiwa ni pamoja na Viwango vya Shirika la Fedha la Kimataifa (IFC), na uzoefu wa angalau miaka 10 katika utendaji wa huduma kama hizo ndani ya Tanzania au kimataifa
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na cheti cha uthibitisho wa kulipa kodi kwa mwaka wa fedha uliopita.
- Maelezo mafupi kuhusu uzoefu na uwezo wa:
- Utekelezaji wa programu za aina hiyo kwa viwango vya fedha vya kimataifa kwa ajili ya miradi mikubwa ya miundombinu nchini Tanzania.
- Kusimamia miradi mikubwa na wakandarasi washirika.
- kufanya kazi kwa kushirikiana na serikali za mitaa na sekta binafsi.
- Wafanyakazi waliopendekezwa kufanya kazi kwenye Mradi huu na ujuzi na uzoefu wao katika kutekeleza programu za aina hii.
- Inashauriwa, mwonyesha nia atume maombi ya kusajiliwa na kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia ya kutekeleza shughuli za progamu.
- Kuzingatia Kanuni za maudhui ya ndani, 2017 na ufafanuzi wa Kampuni ya Ndani

**Mawanda haya yanaweza kugawanywa kimkoa au kiutalaam na KAMPUNI inaruhusu Wazabuni kuwasilisha pendekezo kwa ajili ya kipengele kimoja, kadhaa au vyote.**

Taasisi zenye nia ya kuleta maombi na ambazo zina uwezo na rasilimali za kutekeleza shughuli au kazi zilizoorodheshwa hapo juu zinapaswa kueleza nia yao pamoja na kuambatanisha pamoja na nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwa **eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa wa barua pepe 20 Mb) saa au kabla ya saa **11** jioni za Afrika Mashariki (EAT) tarehe **10 Disemba 2021.** Kichwa cha Habari cha barua pepe ni **0010007287.**

**Muhimu: Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na taasisi zitakazoonyesha nia iii kutengeneza orodha ya taasisi za awali zenye vigezo vinavyotakiwa. Taasisi zitakazokidhi vigezo iu ndiyo zitapokea na kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA) pamoja na mwaliko wa kuwasilisha zabuni katika kuendeleza mchakato wa zabuni. Maelezo yote ya kuonyesha nia yanapaswa kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza.**

EAST AFRICAN
CRUDE OIL
PIPELINE

## OMBI LA KUONESHA NIA UTENEGENEZAJI NA USAMBAZAJI WA MILANGO
## KUMBUKUMBU: 0010007286

Kampuni ya Kimataifa ya Mafuta na Gesi ya TotalEnergies East Africa Midstream B.V, inaalika taasisi zenye weledi na uzoefu kuonesha nia ya kutoa huduma ya Utengenezaji na Ugavi wa Milango katika Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini ya ardhi litakalovuka mipaka ya nchi mbili na litakalosafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika masoko ya Kimataifa. Bomba hili litaanzia Kabaale katika wilaya ya Hoima nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania. Urefu wa Bomba ni kilomita 1,443, kati ya hizo, kilomita 1,147 zitakuwa Tanzania, ambapo bomba hilo litapita kwenye mikoa minane (8) ambayo ni Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara, na Tanga; bomba la mafuta pia litapita kwenye Halmashauri za Wilaya 27 na vijiji 231.

**MAELEZO MAFUPI KUHUSU MAWANDA YA HUDUMA:**

EACOP inahitaji huduma za mtengenezaji mwenye uzoefu na mwenye sifa nzuri kutoa huduma za Utengenezaji na Ugavi wa Milango kutoka kwa mbao aina ya 'Mpodo' au aina nyingine itakayoidhinishwa.

**VIWANGO:**

Nyenzo, uzalishaji na uunganisho wa muundo wa mbao utazingatia viwango vifuatavyo: BS 4978 – Uainisho wa Nguvu ya Kuonekana ya Mbao; BS 5268 - Matumizi ya Kimuundo ya Mbao; BS 6446 - Maelezo ya Utengenezaji na Ugandisho wa Mbao.

Masahihisho ya hivi punde kama yalivyorekebishwa mara kwa mara na Taasisi ya Viwango ya Uingereza yatatumika na MTENGENEZAJI atahakikisha kwamba masahihisho na marekebisho yote ya hivi punde zaidi yametolewa kwa KAMPUNI.

**VIPIMO:**

Mlango wa paneli nene wa 40mm ukubwa wa jumla wa 900 x 2100mm juu, unaojumuisha 120 x 40mm staili, reli za juu, za kati na za chini katika paneli mbili za chini na za juu na fremu ya mlango nene 100 x 45mm; pamoja na vifungio vyake husika kama yalivyotengenezwa na 'ASSA ABLOY' au kampuni nyingine yenye ubora unaofanana (bawaba za kitako cha shaba,pamoja na kitasa cha leva mbili).

Mlango wa paneli nene wa 40mm ukubwa wa jumla wa 800 x 2100mm juu, unaojumuisha 120 x 40mm staili, reli za juu, za kati na za chini katika paneli mbili za chini na za juu na fremu ya mlango nene 100 x 45mm; pamoja na vifungio vyake husika kama yalivyotengenezwa na 'ASSA ABLOY' au kampuni nyingine yenye ubora unaofanana (bawaba za kitako cha shaba,pamoja na kitasa cha leva mbili).

**VIGEZO MUHIMU:**

- MSAMBAZAJI atakuwa na uwezo wa kiwango cha chini cha uzalishaji cha milango 180 kwa mwezi ili kukidhi kiwango kitakachohitajika na KAMPUNI. KAMPUNI inategemea kuwa na uhitaji wa angalau milango 1500 kwa jumla, kwa kiwango kilichoainishwa hapo juu cha milango 180 kwa mwezi.
- KAMPUNI inahifadhi haki ya kuthibitisha utengenezaji wa milango itakonayo na mbao aina ya 'Mpodo' au aina nyingine ambazo zitakazoidhinishwa katika eneo la Mtengenezaji kulingana na mfumo wa usimamizi wa ubora sawasawa na viwango vilivyoainishwa.
- Hakuna nyenzo au viambatisho vitatumika katika utengenezaji hadi kibali cha awali cha matumizi yake kitolewe na KAMPUNI; wala mabadiliko yoyote katika asili, ubora, aina, na aina, chanzo cha usambazaji hakitafanywa bila ruhusa ya KAMPUNI.
- Kwa ombi, nyaraka za ubora wa bidhaa zinazotolewa zinapaswa kuwasilishwa na mtengenezaji kupitia vyeti vya kufanya kazi kulingana na viwango vinavyotumika. Rekodi zote za matokeo ya vipimo vya ubora zitahifadhiwa na mtengenezaji kwa marejesho yajayo.
- Kabla na baada ya kutoa zabuni kwa Mtengenezaji, KAMPUNI ina haki ya kukagua uwezo wa upimaji na kushuhudia majaribio yaliyofanywa katika kituo cha Maabara cha Mtengenezaji kutathmini ubora wa bidhaa kulingana na viwango vinavyotumika.
- KAMPUNI itateua mwakilishi kushuhudia majaribio yote yaliyofanywa katika kituo cha maabara cha Mtengenezaji na mwakilishi atawasilisha matokeo yote ya mkandarasi/mzabuni husika & KAMPUNI kwa kujitegemea. KAMPUNI ina haki ya kuidhinisha Bidhaa kulingana na ripoti za majaribio ya ubora kabla ya kupelekwa kwenye eneo la ujenzi.
- Madirisha na maunzi yake yote yatakuja na dhamana ya vifaa na utengenezaji kwa muda wa miezi 12 tangu tarehe ya kukabidhi.

**VIGEZO MUHIMU VYA KUZINGATIA:**

Taasisi zitakazoonesha nia zinaalikwa kuambatanisha maombi yao pamoja na taarifa zifuatazo:

- Uzoefu, utendaji, na uwezo katika kutekeleza kazi zilizoainishwa chini ya upeo wa kazi, kwa kiwango kikubwa nchini Tanzania, kwa kufuata viwango vya kitaifa na kimataifa (ikiwa ni pamoja na Viwango vya Shirika la Fedha la Kimataifa (IFC), na uzoefu wa angalau miaka 15 katika utendaji wa huduma kama hizo ndani ya Tanzania au kimataifa
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na cheti cha uthibitisho wa kulipa kodi kwa mwaka wa fedha uliopita.
- Maelezo mafupi kuhusu uzoefu na uwezo wa:
- Utekelezaji wa programu za aina hiyo kwa viwango vya fedha vya kimataifa kwa ajili ya miradi mikubwa ya miundombinu nchini Tanzania.
- Kusimamia miradi mikubwa na wakandarasi washirika.
- kufanya kazi kwa kushirikiana na serikali za mitaa na sekta binafsi.
- Wafanyakazi waliopendekezwa kufanya kazi kwenye Mradi huu na ujuzi na uzoefu wao katika kutekeleza programu za aina hii.
- Inashauriwa, mwonyesha nia atume maombi ya kusajiliwa na kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia ya kutekeleza shughuli za progamu.
- Kuzingatia Kanuni za maudhui ya ndani, 2017 na ufafanuzi wa Kampuni ya Ndani

**Mawanda haya yanaweza kugawanywa kimkoa au kiutalaam na KAMPUNI inaruhusu Wazabuni kuwasilisha pendekezo kwa ajili ya kipengele kimoja, kadhaa au vyote.**

Taasisi zenye nia ya kuleta maombi na ambazo zina uwezo na rasilimali za kutekeleza shughuli au kazi zilizoorodheshwa hapo juu zinapaswa kueleza nia yao pamoja na kuambatanisha pamoja na nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwa **eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa wa barua pepe 20 Mb) saa au kabla ya saa **11** jioni za Afrika Mashariki (EAT) tarehe **08 Disemba 2021.** Kichwa cha barua pepe ni **0010007286.**

**Muhimu: Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na taasisi zitakazoonyesha nia iii kutengeneza orodha ya taasisi za awali zenye vigezo vinavyotakiwa. Taasisi zitakazokidhi vigezo iu ndiyo zitapokea na kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA) pamoja na mwaliko wa kuwasilisha zabuni katika kuendeleza mchakato wa zabuni. Maelezo yote ya kuonyesha nia yanapaswa kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza.**

# Makalla apiga 'stop' bomoabomoa Mbweni

**Maulid Mmbaga na Frank Monyo**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, amesimamisha bomoabomoa iliyokuwa ikiendelea kwa wananchi waliovamia eneo la serikali mpakani mwa Mbweni na Bunju A, mkoani hapo, hadi muafaka wa pamoja utakapopatikana.

Alitoa maelekezo hayo jana alipotembelea eneo hilo akiongozana na kamati ya ulinzi na usalama ya mkoa, na inadaiwa kwamba ubomoaji wa makazi hayo ulianza kutekelezwa Novemba 22, mwaka huu, jambo lililosababisha mgogoro kwa wananchi wa eneo hilo.

Kutokana na sintofahamu iliyojitokeza, Makalla alihidi kutuma timu ya wataalamu kutoka Wizara ya Ardhi, Halmashauri ya Kinondoni, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na viongozi wa wananchi hao ili kutafuta suluhu ya pamoja ya kumaliza mgogoro huo.

"Zoezi hili halitafanyika tena, pabaki kama palivyo hakutakuja tena kuendelea na jambo lolote, watakuja watu, nyinyi muungane na hiyo timu kutoa ushirikiano ili eneo hili haki itendeke, nisisikie fujo kwani mkiendelea litabaki hivyo.

"Niwaombe kwa hali ilivyo kwa sasa na nyinyi muwe watulivu ili tuitafute suluhu mkubali niwatume watu, mshirikiane, mtusikilize tuende tukapate ile suluhu ya mwisho maana na nyie mna mapendekezo yenu," alisema Makalla. Kadhalika, alisema baada ya suala hilo kukamilika na kufikishiwa taarifa na timu aliyoituma, atafika eneo husika kutoa tamko kulingana na taarifa atakayopatiwa ili kumaliza mgogoro huo.

Alitoa agizo kwa Jeshi la Polisi kuchunguza vijana wanaodaiwa kuwakamata kutokana na kuanzisha vurugu katika eneo hilo na watakapobaini kuwa hawajasababisha madhara wawaachie ili na wao wawe sehemu ya suala linaloendeshwa sehemu hiyo.

"Muwaachie vijana hao warudi na eneo hili liendelee kuwa tulivu mpaka hapo tutakapopata hatima yake, Ijumaa (leo) wataalamu watakuja wafanye kazi vizuri toeni ushirikiano tusichelewe na wale waliokuwa na vijumba karibu wapikieni na chakula ili wasikitafute mbali," alisema Makalla.

Kwa upande wa wananchi wanaodaiwa kuvamia eneo hilo akiwamo Salum Hashimu, aliiomba serikali kuwaangalia wakati suala hilo likiendelea.




Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Dk. Mashimba Ndaki, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, wakati akiwasilisha taarifa ya mafanikio na mwelekeo katika sekta ya mifugo na uvuvi, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# TotalEnergies yaikuna serikali kumwaga ajira, ujenzi viwanda

**Na Pascal Mayala**

SERIKALI imeipongeza kampuni ya mafuta ya TotalEnergies, kwa kuunga mkono juhudi za Tanzania ya viwanda kwa kujenga viwanda, kutoa ajira, na kuleta teknolojia kwa Watanzania.

Imesema kabla ya ujenzi wa kiwanda cha vilainishi, Tanzania ilikuwa inaagiza vilainishi kwa sababu haikuwa na kiwanda cha kutosheleza soko, lakini sasa kupitia TotalEnegies, Tanzania inajitosheleza kwa vilainishi na ziada inauzwa nje, hivyo kuokoa fedha nyingi za kigeni, inayotumika kuagiza nje pamoja na kupata fedha nyingi za kigeni.

Pongezi hizo zilitolewa na Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaudi Kiguhe, aliyekuwa mgeni rasmi, kwenye uzinduzi wa vilainishi vipya vya magari na mitambo vya kampuni ya TotalEnergies, uliofanyika juzi jijini Dars es Salaam.

Naibu Waziri alisema vilainishi hivyo vinatumia teknolojia ya kisasa kuvitengeneza, lakini sasa Watanzania wamejengewa uwezo sio tuu kwa kupatiwa fursa za ajira bali pia kupatiwa uwezo wa teknolojia kutoka kwao kuja nchini.

Pia aliiongeza kuwa TotalEnergiy mpaka sasa, ndiye mwekezaji mkubwa Tanzania kupitia mradi wake wa EACOP kuliko mradi mwingine wowote.

Kampuni ya TotalEnergies Marketing Tanzania Limited ambayo awali ilijulikana kama Total Tanzania Limited, mezindua vilainishi hivyo kama sehemu ya maadhimisho ya wiki ya huduma kwa wateja ya TotalEnergies kwa mwaka 2021, yenye kaulimbiu ya 'Tujienge kesho pamoja'.

Hii ni awamu ya tatu ya wiki ya huduma kwa mteja ya TotalEnergies tangu ianzishwe mwaka 2019. TotalEnergies inaendelea kuonyesha dhamira yake kwa Tanzania kwa kuwakaribisha wateja wao ili kushiriki maono yao ya mustakabali wa kampuni ya TotalEnergies Marketing Tanzania Limited nchini.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo, Mkurugenzi Mkuu wa kampuni, Jean-Francois Schoepp alisema kuwa, "Kama baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere aliwahi kusema kuwa "Ikiwa maendeleo ya kweli yatatokea, ni lazima wananchi washirikishwe." Pia tunaamini kwamba TotalEnergies Marketing Tanzania Limited itaendelea kukuwa zaidi endapo tutawashirikisha wateja wetu na kuwa tayari kukidhi mahitaji kikamilifu."

Wafanyakazi wa TotalEnergies Marketing Tanzania Limited wakiongozwa na mkurugenzi mkuu, Jean-Francois Schoepp, walitoa huduma kwa wateja waliotembelea kituo cha TotalEnergies East Oysterbay Jumatatu na kupata fursa ya kusikiliza maoni ya wateja, kuboresha mahusiano na wateja wao kwa nia ya kuziba mapengo yoyote yaliyewepo na kuweza kujenga TotalEnergies Marketing Tanzania Limited kwa pamoja na wateja wao.

# Bandari ya uvuvi sasa kujengwa Kilwa Masoko

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi inaendelea kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa bandari ya uvuvi kupitia mtaalamu mwelekezi ambaye ni Kampuni ya M/S Sering Ingegneria ya Italia kwa gharama ya Sh. 1,421,041,703.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, alibainisha hayo jana alipokuwa akitoa taarifa ya mafanikio ya sekta ya mifugo na uvuvi kwa waandishi wa habari katika kipindi cha miaka 60 ya uhuru wa Tanganyika.

Alisema serikali tayari imechagua eneo la Kilwa Masoko kwa ajili ya kujenga bandari ya uvuvi.

"Katika mwaka huu wa fedha 2021/2022, serikali imetenga kiasi cha Sh. bilioni 50 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa bandari hiyo mara baada ya kukamilika kwa upembuzi yakinifu.

Aidha, alisema jitahada za kutafuta wawekezaji wa kujenga miundombinu mingine ya uvuvi katika eneo hilo zinaendelea vizuri.

Pia, alisema serikali inaendeleza jitihada za kuthibiti ubora na usalama wa samaki na mazao ya uvuvi ili kulinda soko la ndani na nje ya nchi.

Alisema jitihada hizo ni pamoja na kuanzisha Maabara ya Taifa ya Uvuvi Nyegezi mnamo mwaka 1997.

"Ndugu wanahabari, vilevile, katika kuimarisha ubora wa mazao ya uvuvi katika mnyororo wa thamani, serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya uvuvi ikiwamo ujenzi na ukarabati wa mialo ya kupokelea samaki na masoko," alisema Ndaki.

Alisema hadi sasa kuna jumla ya mialo ya kisasa 33 na masoko 17 ikilinganishwa na mwaka 1961 ambapo hapakuwa na mialo iliyoboreshwa na masoko ya kisasa.

Pia, alisema kufuatia juhudi hizo, kiasi cha mazao ya uvuvi yanayouzwa nje ya nchi yameendelea kuongezeka kutoka tani 17,269.90 na samaki wa mapambo 4,116 zenye thamani ya Sh. bilioni 11.93 mwaka 1995 hadi tani 40,477.97 na samaki wa mapambo 128,316 zenye thamani ya Sh. bilioni 386.37 mwaka 2020.

Aidha, alisema mauzo hayo yaliingizia Taifa Sh.milioni 629.57 mwaka 1995 ikilinganishwa na Sh. bilioni 21.67 mwaka 2020 kama mrahaba.

Vilevile, alisema serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi ya kuvutia uwekezaji katika sekta ya uvuvi kwa kufanya mapitio ya mara kwa mara ya kuboresha sera, sheria, kanuni na taratibu.

Alisema wizara imeanzisha Dawati la sekta binafsi kwa ajili ya kutoa elimu, kuwaunganisha wadau wa uvuvi na taasisi za kifedha ili kuwawezesha kupata mikopo yenye masharti nafuu.

Alifafanua kuwa kutokana na jitihada hizo, idadi ya viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi imeongezeka kutoka viwanda vinne vilivyokuwa na uwezo wa kuzalisha tani tatu mwaka 1992 hadi 15 vyenye kuzalisha tani 40 hadi 60 kwa siku kwa mwaka 2021.

Hata hivyo, alisema tangu kuanzishwa kwa Mamlaka ya uvuvi katika kina kirefu cha bahari (DSFA) hadi mwaka 2021/2022, jumla ya meli za uvuvi 502 zimepatiwa leseni zenye thamani ya Sh. 24,314,736,449 ambapo jumla ya tani za ujazo 67,437.90 za samaki zilivuliwa katika EEZ ya Tanzania kwa wastani wa tani 6,130.7 kwa mwaka.

# Songas yaipa serikali gawio bil. 21/-

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Songas Limited, inayojihusisha na uzalishaji wa umeme kwa kutumia nishati ya gesi, imeilipa serikali Sh. bilioni 21.2 kama gawio la hisa zake katika kampuni hiyo.

Kampuni ya Songas Limited ni mshirika wa serikali katika kufikia mahitaji ya nishati ya umeme Tanzania na umiliki wake unajumuisha taasisi za nishati - Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) asilimia 28.69, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) asilimia 9.56 na Tanzania Development Finance Company Limited (TDFL) asilimia 7.65 pamoja na Globeleq asilimia 54.1, kampuni binafsi ya uzalishaji wa umeme yenye shughuli zake barani Afrika.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni hiyo, Anael Samuel, alisema mwaka 2021, TANESCO itapokea Sh. bilioni 4.4, huku TPDC ikipokea Sh. bilioni 11 na TDFL Sh. bilioni 3.5 bilioni , na kwamba, kila gawio litakatwa kodi ya kiasi ni baada ya kukokotoa kodi ya zuio.

Alisema Songas imelipa jumla ya Sh. bilioni 157 tangu kuanzishwa kwake kama gawio kwa serikali na taasisi zake.

"Ukame unaoendelea nchini unaonyesha kuwa mchanganyiko wa nishati inayosaidia umeme wa maji ni muhimu kwa uendelevu wa sekta ya nishati nchini," alisema Anael.

Aliongeza kuwa mtambo wa umeme wa Songas Ubungo ni wa kiwango cha kimataifa na unaofanya kazi kwa asilimia 109 ya uwezo wake.

"Songas inachangia takribani asilimia 20 ya nishati nchini na sasa inaongoza kwa kuzalisha nishati kwa bei nafuu katika ukanda wa Afrika Mashariki kwa kwa kutumia nishati ya gesi asilia. Mahitaji ya umeme nchini Tanzania yanakadiriwa kukua kwa asilimia 10 -15 kwa mwaka, na kampuni hiyo ina nafasi ya kipekee ya kusaidia ukuaji wa viwanda nchini."



Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa Tanzania, Mohamed Ali Ahmed, akizungumza na viongozi wanawake kutoka vyama 19 nchini, katika mkutano uliowakutanisha kujadili nafasi ya uongozi ya mwanamke, mkoani Dar es Salaam juzi. Kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Lilian Liundi na Mratibu wa Taifa ULINGO, Dk. Ave Maria Semakafu. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# Magereza Rukwa yajenga mabweni ya wafungwa

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

JESHI la Magereza mkoani Rukwa limejenga mabweni matatu katika Gereza la Mahabusu Sumbawanga yatakayokuwa na uwezo wa kuchukua wafungwa 200 kwa wakati mmoja na kuondoa mrundikano wa wafungwa katika gereza hilo.

Akizindua mabweni hayo jana, Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Joseph Mkirikiti, alisema mabweni hayo yatasaidia kupunguza mrundikano wa wafungwa uliokuwapo awali kutokana na mabweni machache.

Alisema gereza hilo lilianzishwa mwaka 1927 na wakoloni likiwa na uwezo wa kuchukua wafungwa 200, lakini mpaka sasa linachukua wafungwa 422 kitendo kilichokuwa kikisababisha msongamamo.

Aidha, alitoa wito kwa vyombo vya utoaji haki ikiwamo mahakama na Jeshi la Polisi kuharakisha michakato ya upelelezi na usikilizwaji wa mashauri mahakamani ili watuhumiwa waweze kupata haki zao mapema hatua inayosaidia kupunguza msongamano magerezani.

"Vyombo vya kutoa haki vifanye kazi zake haraka na kwa uaminifu ili haki itendeke na wasio na hatia basi wasiendelee kukaa mahabusu bali waruhusiwe kurejea uraiani kuendelea na ujenzi wa taifa," alisema.

Kwa upande wake Mkuu wa gereza hilo Mrakibu wa Magereza, Melkior Komba, alisema mradi huo umegharimu Sh. milioni 187 kati ya hizo Sh. milioni 62 zilitolewa na Kamishna Jenerali wa Magereza huku wadau wakichangia Sh. milioni 124.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Sumbawanga, Sebastian Waryuba, alisema kwa kuboresha mahala pa kulala wafungwa isiwe ni kigezo cha watu kufanya makosa na kukimbilia huko, bali waendelee kuelimishwa ili waepuke vitendo vya kihalifu na uvunjifu wa amani kwa kufanya makosa yanayosababisha kuwekwa mahabusu au kifungoni.

# Kijaji awaasa wanafunzi vyuo vikuu

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Ashatu Kijaji, amewataka wanafunzi wa vyuo vikuu nchini kurejea kwenye uzalendo kwa nchi yao, miiko na maadili mema ya Kitanzania yatakayowaongoza kufikia mafanikio katika kuwatumikia wananchi.

Dk. Kijaji alisema hayo wakati wa mkutano wa Baraza la Wahitimu waliosoma Chuo Kikuu Mzumbe, mkoani hapa.

Alisema mafanikio yoyote ikiwamo suala la uongozi lazima kutanguliza mbele uzalendo na kuonyesha mfano kwa watu unaowaongoza.

Dk. Kijaji pia aliwataka vijana wanaosoma kwenye Chuo Kikuu Mzumbe kuwa mfano wa kuigwa wanapokuwa chuoni na wanapomaliza masomo yao kwa kujitoa kuwatumikia wananchi kwa nguvu zao zote.

"Wapo baadhi ya wazazi na watu wengi wana mtazamo hasi kwa watoto wao wakifika hatua ya kwenda chuo, wanawaza huko kuna mambo mabaya na wazazi wengine kuwazuia," alisema Dk. Kijaji.

"Niwaeleze mimi nimesoma hapa Chuo Kikuu Mzumbe nikapata mume nikiwa chuoni, nilijua kilichonileta nikamwekea mtazamo wangu, mume akanielewa na tukamaliza wote chuo mpaka sasa tunaendelea vyema," alisisitiza Dk. Kijaji.

Alisema, mtazamo huo hasi unaweza kuondolewa na wanafunzi wenyewe hususani wa kike kwa kujikita katika uzalendo na maadili ya kitanzania.

Kadhalika, alisema viongozi wengi wanaofanya kazi nzuri nchini wengi ni zao la chuo hicho ambao ni tegemeo kubwa la taifa.

"Rais Samia Suluhu Hassan ni miongoni mwa zao la Mzumbe na amekuwa mfano wa kuigwa amefanya mambo makubwa tangu aingie madarakani na Mzumbe tunatakiwa kujivunia hilo na tunaona mambo mazuri yanayofanyika," alisisitiza Dk. Kijaji.

Naye Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Jamal Kassim Ali, alisema ili mtu yeyote aweze kufanikiwa ni lazima awe na malengo na kujiamini na kufanya maamuzi magumu pale anapoona inabidi kwa maslahi ya wengi.

Alitoa wito kwa vijana kuwa pamoja na ndoto walizonazo katika maisha, lazima wazifunganishe katika tija kwa kuangalia maslahi ya taifa kwanza.

Pia, alisema wanafunzi wanapokuwa vyuoni wakumbuke wanawajibu wa kulipa deni baada ya kumaliza masomo yao kwenda kuwatumikia wananchi kwa weledi, bidii na nidhamu wakitambua wamefikishwa hapo kutokana na kodi za wananchi.

Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Profesa Lughano Kusiluka, alisisitiza umuhimu wa kupata maoni ya wahitimu mbalimbali waliopo kwenye mamlaka hali itakayoibua mafanikio ya chuo na wanafunzi kwa ujumla.

# Mil. 130/- zapatikana harambee kutunisha mfuko wa Ukimwi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

ZAIDI ya Sh. milioni 130 zimepatikana kwenye harambee iliyofanyika wakati wa matembezi ya hisani iliyofanyika jijini Mbeya, kwa ajili ya kutunisha Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti Ukimwi nchini (ATF).

Matembezi hayo ya hisani yalifanyika jana wakati wa uzinduzi wa wiki ya maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani yaliyoanzia katika eneo la Mwanjelwa jijini Mbeya na kuishia katika Uwanja wa Ruanda Nzovwe kwa kushirikisha wadau mbalimbali.

Naibu Spika Dk. Tulia Ackson ambaye alikuwa mgeni rasmi kwenye matembezi hayo alisema baadhi ya wadau walitoa fedha taslimu na wengine waliahidi kuchangia kwa njia ya mitandao ya simu na benki.

Alisema kati ya fedha hizo Sh. milioni 100 zilichangwa na taasisi mbili ambazo ni mgodi wa dhahabu wa Geita Gold Mine na Kampuni ya Star Time ambayo kila moja lilichangia Sh. milioni 50.

Aliwataka wananchi kuendelea kuchangia mfuko huo na kwamba kwa watakaochangia michango mikubwa watatambuliwa na watapatiwa vyeti na Rais Samia Suluhu Hassan kwa kupatiwa vyeti maalumu.

"Lakini nawasihi wananchi hasa vijana wajitokeze kupata huduma mbalimbali zinazotolewa hapa, kuna mabanda mbalimbali hapa yanayotoa huduma za kiafya hivyo naomba mchangamkie huduma hizi," alisema Dk. Tulia.

Mwenyekiti wa Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti Ukimwi (ATF), Jenard Lazaro, alisema katika maadhimisho hayo huduma mbalimbali za kiafya zitakuwa zinatolewa ikiwamo upimaji wa afya, utoaji wa elimu ya Ukimwi pamoja na afuu mbalimbali za kuudhibiti.

Alisema mfuko huo ulianzishwa na serikali kwa lengo la kuhakikisha Tanzania inajitegemea kwenye mapambano dhidi ya Ukimwi pamoja na kuhakikisha inawashirikisha wadau wake kwenye mapambano dhidi ya Ukimwi.

Alisema pamoja na kuanzishwa kwa mfuko huo, wanakabiliwa na uhaba wa fedha kutokana na idadi ndogo ya wadau wanaojitokeza kuchangia fedha za kutunisha mfuko huo.

"Ili kuutunisha vizuri mfuko huu, tunaiomba serikali ianzishe tozo maalumu kwa ajili ya kukusanya fedha badala ya kuendelea kuchangishana kwa njia hii tunayotumia," alisema Lazaro.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Taifa ya kudhibiti Ukimwi (TACAIDS), Dk. Leonard Maboko, alisema kwa sasa wamewekeza nguvu kubwa zaidi kwenye utoaji wa elimu kwa jamii ili kukabiliana na maambukizi mapya.

Alisema mapambano dhidi ya maambukizi mapya ya VVU yanashirikisha wadau mbalimbali wakiwamo sekta binafsi pamoja na kuna idara katika wizara mbalimbali ambazo zinashughulika na Ukimwi.

Maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani kitaifa yatafanyika jijini hapa na mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Rais Samia Suluhu Hassan..




Meneja Masoko na Mawasiliano Msaidizi wa Benki ya Exim, Mariamu Mwapinga (kushoto), akiwaonyesha waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, zawadi kubwa ya gari aina ya Toyota Vanguard, itakayotolewa kwa mshindi wa kampeni ya 'Weka Mkwanja Tukutoe!' inayolenga kuhamasisha Watanzania kujiwekea amana kupitia benki hiyo. Wengine ni ofisa kutoka Bodi ya Michezo ya Kubahatisha, Neema Tatock (wapili kushoto) na maofisa wa benki hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Washindi droo Exim wajizolea fedha, gari

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Exim imetangaza washindi wa droo ya kwanza ya kampeni ya 'Weka Mkwanja Tukutoe!'inayoendeshwa na benki hiyo, ikilenga kuhamasisha Watanzania kujiwekea amana, huku wakinyakua zawadi mbalimbali ikiwamo fedha taslimu na gari aina Toyota Vanguard.

Akitangaza washindi wa droo ya kwanza ya kampeni hiyo iliyofanyika jana jijini Dar es Salaam, Meneja Masoko na Mawasiliano Msaidizi wa Benki hiyo, Mariam Mwapinga, alisema jumla ya washindi sita walipatikana kupitia droo hiyo na kujishindia zawadi ya shilingi milioni sita fedha taslimu.

"Katika droo ya leo jumla ya washindi sita wamepatikana na wameweza kujishindia zawadi za fedha taslimu shilingi milioni sita. Washindi hawa sita watakabidhiwa zawadi zao katika maeneo yao waliopo na tutaendelea na droo kama hizi kila mwezi na washindi wataendelea kuingia kwenye droo itakayowawezesha kushinda zawadi kubwa ya gari aina ya Toyota Vanguard."

"Wateja wetu wa sasa na wale wapya watakuwa kwenye nafasi ya kujishindia zawadi hizi kila wakapojiwekea akiba ya kuanzi shilingi 500,000 na kuendelea. Kadili wanavyojiwekea amana kubwa zaidi ndivyo wanavyojiweka kwenye nafasi ya kushinda zawadi kubwa zaidi," alisema Mariam wakati wa droo hiyo iliyohudhuriwa pia na mwakilishi kutoka Bodi ya Michezo ya Kubahatisha nchini.

Akifafanua zaidi kuhusu kampeni hiyo, Mariam alisema inalenga kuleta mabadiliko kwenye mtazamo wa uhifadhi wa amana miongoni mwa Watanzania kutoka kuhifadhi pesa majumbani na badala yake wazihifadhi kupitia benki hiyo kwa usalama wa fedha zao sambamba na faida nyingine nyingi ikiwamo riba.

"Lengo si tu kuhamasisha Watanzania kujenga utamaduni wa kujiwekea amana, tunachohitaji ni kuona kwamba Watanzania wengi wanajiwekea amana zao sehemu salama ili kujiendeleza kukua kiuchumi ndio maana tumejipanga kuwahamasisha watumie akaunti zetu mbalimbali ikiwamo akaunti ya mshahara inayotumika kwa matumizi mbalimbali ya kila siku," alisema.

# Wataka magari yanayopelekwa TBS kukaguliwa yasikamatwe

**Mwandishi Wetu**

BARAZA la Taifa la Biashara (TNBC) limefanya mkutano wa pamoja wa viongozi wa sekta binafsi na sekta ya umma jijini Dar es Salaam kuhusu ukaguzi wa magari kabla au baada ya kupandishwa melini kusafirishwa kuja Tanzania yakiwa bado yamo katika mchakato wa kukaguliwa na TBS au kupelekwa mabohari ya jastamu yasikamatwe na taasisi husika.

Mkutano huo umeazimia kwamba mifumo yote ya ukaguzi wa magari kabla ya kupandishwa na baada ya kushushwa melini kutumika. Pia umeazimia kuboresha mitambo na mashine inayotumika katika ukaguzi wa magari katika karakana ya TBS au mipaka ya Tanzania.

Azimio hilo la kikao limetolewa baada ya mkutano Novemba 19, mwaka huu uliojadili utekelezaji wa azimio la mkutano wa 12 wa TNBC. Viongozi na wawakilishi wa sekta ya umma na binafsi wameazimia kwamba itumike mifumo yote miwili ya kukagua magari yanayoingia Tanzania, yaani ukaguzi wa nje ya nchi kabla ya magari kupandishwa melini na ukaguzi wa ndani ya nchi baada ya magari kushushwa melini (bandarini).

Taarifa ya mkutano ilieleza kuwa kikao kimeelekeza kwamba mpango kazi wa utekelezaji wa maazimio hayo uandaliwe na kuanza kutekelezwa.

TNBC iliitisha kikao hicho na wajumbe walikuwa ni Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Biashara (TNBC), Dk. Godwill G. Wanga, Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Dotto James, Mwenyekiti wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania, Angelina Ngalula, Karani wa Baraza la Mawaziri, Nsubili Joshua, Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Dk. Athuman Ngenya na wadau wengine wa sekta binafsi na sekta ya umma.

Kikao hicho kiliazimia kuandaa na kuanza kutekeleza mpango kazi wa utekelezaji wa maazimio yaliyofikiwa.



Ukurasa 12

Samia alivyosawazisha tatizo lililokwaza uwekezaji nchini




Ukurasa 13

Ushiriki wa jamii unatakiwa sana katika vita biashara dawa kulevya

BUFE

IJUMAA NOVEMBA 26, 2021

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



Ukurasa 14

MPANGO MAENDELEO & UCHUMI BLUU...

## TAFIRI yafungulia Mwanza njia kupitia vizimba samaki Viktoria

# Mamlaka habari zatafsiri kinachonaswa na 'CCTV' zake unyanyasaji jinsia kazini

- Wasomi wao wakokotoa ya utafiti

**Na Jenifer Gilla**

SEHEMU ya kwanza ya makala hii imeripoti unyanyasaji kijinsia ndani ya vyombo vya habari, kukiwapo ushuhuda walioguswa moja kwa moja, pia wasimamizi wao wakianika uhalisia.

Nipashe sasa inahamia wadau wakuu wa sekta wanavyozungumzia mustakabli, ikianza na utafiti wa shirika la WAN-IFRA Women in News kuhusu unyanyasaji kijinsia katika vyombo vya habari.

Hapo unaonyesha nusu ya wanawake katika vyumba vya habari Afrika wanafanyiwa unyanyasaji kijinsia, lakini wanaoripoti wachache wakikatishwa tamaa na hatua nyepesi zinazochukuliwa, ikiwamo kuishia kuonywa.

Mratibu wa WAN-INFRA/women Tanzania Dk. Joyce Bazira, anasema kuwapo sera katika vyombo vya habari kutawapa ujasiri wanahabari kutoa taarifa wanaponyanyaswa kijinsia.

" Wapo waandishi wanaotamani kuripoti matukio ya unyanyasaji, lakini wanahofia kukosa ajira zao kwa kuwa hakuna sera zinazowalinda ndani. Hivyo, ni muhimu vyombo hivyo vikafikiria kutengeneza sera za ndani" anasema.

Dk. Bazira, mkongwe katika vyumba vya habari, mshiriki utafiti na mtoaji elimu kuhusu unyanyasaji kupitia asasi kama vile WAN-IFRA / Women in News na Chama cha Wanadishi wa Habari Wanawake (TAMWA), anashauri sera hiyo iambatane na mambo kadhaa.

Anayataja kuwa ni elimu, uhamasishaji jamii na undani wake, kuondoa utamaduni uliojengeka kwamba "ni jambo la kawaida, halipaswi kusemwa na jamii."




Msomi huyo anafafanua: "Kuna watu wanafanyiwa unyanyasaji wa kijinsia bila ya kujua wakidhani ni jambo la kawaida. Mfano, unamsalimia mwanamume kwa kumpa mkono, halafu anakutekenya kwenye kiganja. Ule ni unyanyasaji, lakini wengi wanachukulia kama ni hali ya kawaida."

Pia, anataja wanaume wanaonyanyasa pasipo kujitambua wanakosea, kwa sababu ya kukosa elimu sahihi, akitoa mfano anapomkonyeza mwanamke asiye mke wake.

Mwanahabari wa kujitegemea, Christina Stephen, anaungana na Dk.Bazira, akisema wanaogopa kuripoti matukio ya unyanyasaji wa kijinsia ili kulinda maslahi yao.

"Unakuta aliyekufanyia kitendo cha unyanyasaji ni bosi wako na ndiye anaamua habari hii itoke ukurasa gani. Ukienda kumshtaki, anaweza kukuwekea chuki na kukukomoa," anasema Christina, akitaja mbadala unaochukuliwa na anayeonewa ni kuvumilia.

Mwandishi wa habari wa Gazeti la Mwananchi na Mkuu wa Kitengo cha Takwimu, Halili Letea anasema utamaduni na malezi waliojengewa wanawake kuwa baadhi ya mambo hayapaswi kuripotiwa, yanawachangia wasitoe taarifa wanaponyanyaswa, yabaki kuwa siri.

"Hii inawapa mwanya viongozi wa kiume kuendeleza haya matendo machafu, kwa hivyo sera ni muhimu katika vyombo vya habari," anasema

Letea anatoa ushahidi wa mwanahabari wa kike jasiri, aliyetoa taarifa za kunyanyasika kingono faragha ya umbo, hata ofisi yao ikaamua kuongeza idadi ya kamera kunasa vyema matukio aina hiyo ili yachukuliwe hatua.

Mwandishi wa habari wa gazeti moja la jijini Dar es Salaam, Rachel Imanuel (sio jina lake kamili) anakiri kupitia unyanyasi kingono kazini na hakutoa taarifa kwa kuhofia kuweka ajira yake rehani

"Sasa ukishamshitaki bosi itakuwaje? Wakati hakuna sheria ya ndani . Hata sisi waandishi wa habari wa kujitegemea, unaweza kupoteza ajira dakika moja tu. Kukiwa na sheria ya kupinga unyanyasaji katika vyumba vya habari, itatupa nguvu hata sisi kutoa taarifa," anasema Rachel.

### KUTOKA FEMNET

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Kimataifa la Kutetea Haki za Wanawake, (FEMNET), Memory Kachambwa, anasema kukosekana sera ya kushughulikia unyanyasaji kijinsia kazini, kunasababisha vitendo hivyo kuwa endelevu.

Kachambwa anaeleza unyayasaji wa kijinsia kazini ni zao la kukosekana usawa wa mamlaka na dalili zake ni mazingira kama vile malipo ya chini kwa wanawake na wasichana kazini.

"Wanawake wakinyanyasika wanakosa ari ya kufanya kazi, hali inayowafanya kuacha kazi na kuhatarisha uwezeshaji wao wa kiuchumi.

"Hii ina athari kubwa katika shirika zima na inaweza kusababisha kudorora kwa ustawi wa shirika, hivyo sera ya ndani ni muhimu kulinda maslahi ya wanawake hawa," anasema Kachambwa

Mkuu huyo wa FEMNET anazisisitiza nchi za Kiafrika kuidhinisha mkataba wa 190 wa Shirika la Kazi Duniani (ILO) ili kukomesha unyanyasaji kazini akianika kati ya nchi saba duniani zilizoridhia mkataba huo tatu ni za Afrika; Namibia, Somalia na Mauritius.

### WAN-IFRA /Women in News

Mkurugenzi wa shirika WAN -IFRA, kwa nchi za Afrika, Jane Godia, anasisitiza haja ya kuwapo sera yenye viwango, miongozo na taratibu za kushughulikia kesi za unyanyasaji kijinsia endapo zitatokea, ikiwa na ufafanuzi wa hatua za kinidhamu kupopatikana hatia.

" Sera hii itawafungua macho waandishi wa habari wajue kuwa hawastahili kufanyiwa vitendo vya unyanyasaji na ni muhimu sera hii ikumbushwe mara kwa mara kwa wahusika kupunguza au kuondoa kabisa unyanyasaji wa kijinsia," anasema.

Mbobezi huyo wa zaidi ya miaka 20, pia mhariri, mkufunzi kwa wanahabari, anasema unyanyasaji huo unatokea kwa jinsia zote, lakini wanawake ni waaathirika wakubwa kutoka kwa mabosi.

Tathimini ya muundo na utendaji katika vyombo vya habari dhidi ya uhamasishaji wa usawa kijinsia na kupinga udhalilishaji wanahabari wanawake iliyofanywa na TAMWA unaeleza kuwa 25% ya wanawake wanahabari wamenyanyasika kijinsia kwa kurubuniwa kimapenzi; 17.2% kwa picha za mtandaoni; 15.2% shambulio la mwili; 12.4% kulazimishwa ngono na 4.8% walibakwa.

UCHUMI

# Samia alivyosawazisha tatizo lililokwaza uwekezaji nchini

• Ajivunia mafanikio ndani ya muda mfupi • Profesa uchumi aibuka na angalizo lake



Rais Samia Suluhu Hassan, alipokutana na Mhandisi Ahmed El Sewedy, Rais na Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Elsewedy Electric ya nchini Misri, baada ya kuwasili Ikulu Chamwino jijini Dodoma, Agosti mwaka huu. **PICHA: MAKTABA**

**Na Sanula Athanas,** ARUSHA

JUNI 15, mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan alipozungumza na vijana jijini Mwanza, aliweka wazi kuwapo upungufu mkubwa wa ajira zao nchini.

Kimsingi, ni wimbo unaosikika nchini na kwingineko duniani, ingawa uhalisia wake unatofautiana kati ya taifa moja na lingine.

Wakati wa mkutano uliopita wa Bunge la Bajeti, wabunge pia waliibua suala hilo wakianika kinachowasibu vijana waliohitimu masomo, ni kukosekana fursa za ajira kwao.

Alipokuwa mkutanoni jijini Mwanza, Rais Samia alibainisha Tanzania ina jumla ya vijana milioni 20.7 wenye umri kati ya miaka 15 na 35, lakini kati yao asilimia 11.4 ya wenye sifa za kuajiriwa, hawako kazini.

Vilevile, akihutubia kinamama jijini Dodoma Juni, mwaka huu, Rais Samia alitaja idadi ya Watanzania wenye ajira rasmi kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2017 ni wastani wa milioni tatu (takwimu halisi 3,014,106).

Huo ni wastani wa asilimia tano ya Watanzania kwa mujibu wa takwimu za sasa, ndiyo wako kwenye ajira rasmi.

> **“Wananchi wana haki ya kujua matumizi ya fedha zao. Wakishajua matumizi ya fedha hizo, wanakuwa katika nafasi nzuri zaidi ya kufanya ufuatiliaji ambao sasa utaimarisha zaidi uwajibikaji.**

Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) imeripoti Agosti 14, 2019 kiwango cha ajira kilipungua kwenye sekta binafsi kutoka waajiriwa 239,019 mwaka 2016/17 hadi ajira 137,054 mwaka uliofuata, yaani 2017/18.

Rais Samia katika ufafanuzi wake kwa vijana, siku hiyo, aliangukia mtazamo wa wataalamu uchumi, akiwamo Mkuu wa Chuo Kikuu cha Mzumbe kampasi ya Dar es Salaam, Prof. Honest Ngowi, kwamba fursa za ajira serikalini ni finyu na mtazamo mpana uko sekta binafsi.

Pia Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), inataja tathmini ya uhaba wa ajira kitaifa na kiini cha tatizo.

CAG, Charles Kichere, kupitia ripoti ya mwaka 2019/20 iliyowalishwa bungeni Aprili mwaka huu, anasema uwekezaji umepungua na kukwaza ajira.

Anabainisha miradi mipya kwenye Kituo cha Uwekezaji (TIC), ilipungua kwa wastani wa nusu na ndiyo ulikuwa uhalisia wa mwenendo wa ajira nchini miaka mitano iliyopita.

CAG anasema kwa kipindi hicho ajira zilipungua kutoka waajiriwa 63,223 mwaka 2015/16 hadi waajiriwa 32,115 mwaka 2019/20, sawa na asilimia 48.

Takwimu hizo zinatoa taswira inayokinzana na maelekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21) unaoielekeza serikali kuhamasisha, kuwezesha na kuratibu uwekezaji, mabadiliko ya teknolojia, viwanda na biashara nchini.

Ripoti ya CAG inasema kupungua miradi hiyo kumechangiwa na kuwapo mazingira hasi kwenye uwekezaji. Inabainisha Tanzania kuwa ya 141 kati ya 190 kwa vigezo vya mazingira rafiki, kwa uwekezaji na inatajwa kuporomoka kwa asilimia nane katika utengenezaji mazingira rafiki ya uwekezaji kwa miaka mitano iliyopita (2015-2020).

CAG anasema, ni hali inayosababishwa na TIC kutotoa huduma zote stahiki za uwekezaji (one stop centre), ikitoa huduma nne kati ya 11 zinazotakiwa kuwapo.

“Kuna ucheleweshaji wa mrejesho wa maombi ya uwekezaji katika mamlaka husika. Vigezo vya kimataifa vinataka iwe ndani ya siku 14, lakini uhalisia uliopo nchini ni siku 182 hadi 675,” anabainisha.

Ni hali inayotoa tafsiri kitaalamu kwamba, hitaji la wiki mbili, linahitimishwa ndani ya wiki 26 au miezi sita.

CAG anadokeza Tathmini ya Athari za Mazingira inayotekelezwa na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), inachukua muda mrefu kukamilika, wastani wa siku 95.

Vilevile, ananyooshea kidole uhaba wa bajeti, akibainisha upungufu wa nusu ya hitaji halisi Sh. bilioni 45 (asilimia 49 ya mahitaji) na uhaba wa theluthi moja ya watumishi (asilimia 35 ya mahitaji ya watumishi 513) kwa mwaka huo wa ukaguzi.

Kupungua miradi mipya iliyosajiliwa TIC kwa miaka mitano mfululizo kuanzia mwaka 2015/16 hadi 2020/21. CHANZO: Ripoti ya CAG 2019/20.

### JICHO LA PROF. NGOWI

Katika wasilisho lake kuhusu uwazi na uwajibikaji wa kifedha wakati wa Mkutano wa Kimataifa wa Uwazi na Uwajibikaji (ITAC) jijini Arusha wiki iliyopita, Prof. Ngowi anashauri kuzitafutia ufumbuzi dosari zinazokwaza uwekezaji nchini.

Mkutano huo ulioshirikisha viongozi na wataalamu wa masuala mbalimbali yakiwamo ya kiuchumi, uliandaliwa na Taasisi ya WAJIBU.

Prof. Ngowi anasisitiza uwazi kwenye Utoaji vibali vya uwekezaji; ujenzi wa miradi; soko. Pia anasema kuwapo rushwa na kutotabilika kwa sera na sheria, kunasababisha uwekezaji nchini uendelee kuyumba.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Taasisi ya WAJIBU, Yona Killagane, anaunga mkono hoja ya serikali itafute majibu sahihi ya kukabiliana na kuyumba kwa uwekezaji nchini.

Killagane, pia aliishauri serikali kuondoa alichokiita ‘pengo la kibiashara’ kati yake na sekta binafsi. Anasema ni pengo hilo litakaloondolewa kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji miradi ya serikali.

Mwenyekiti huyo, anaishauri serikali iboreshe mazingira ya uwekezaji kutekeleza kikamilifu mpango mkakati wa kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini (Blueprint), ambao haujatekelezwa kikamilifu.

### WAZIRI WA FEDHA

Akifungua mkutano, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, anakiri uwekezaji nchini umeyumba katika miaka ya karibuni na Rais Samia ameshaliona na kuweka mikakati ya kuimarisha eneo hilo.

Anasema, dhamira ni kuhakikisha uwazi na uwajibikaji unakuwapo katika usimamizi wa rasilimali za umma, kwa kuweka wazi takwimu na ripoti zinazohusu rasilimali za taifa.

Anasema mkuu huyo wa nchi anaendelea kuwawajibisha watendaji wa serikali wanaobainika kufuja mali ya umma na wanaoonekana kukwaza uwekezaji nchini.

Mkurugenzi wa Taasisi ya WAJIBU, Ludovick Utouh, katika hilo anampongeza Rais Samia kuanika matumizi ya Sh. trilioni 1.3 zilizokopwa na serikali kutoka Shirika la Fedha Duniani (IMF) kukabiliana na athari za UVIKO-19.

Utouh, aliyewahi kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), pia Mkurugenzi wa Bodi ya Uhasibu na Ukaguzi wa Hesabu (NBAA), anaendelea:

“Wananchi wana haki ya kujua matumizi ya fedha zao. Wakishajua matumizi ya fedha hizo, wanakuwa katika nafasi nzuri zaidi ya kufanya ufuatiliaji ambao sasa utaimarisha zaidi uwajibikaji.”

### MAFANIKIO YA SAMIA

Rais Samia alipohutubia mkutano wa Umoja wa Wanawake (UWT) visiwani Zanzibar, hivi karibuni, alisema katika kipindi kilichopita Tanzania ilipata mafanikio makubwa katika nyanja mbalimbali zikiwamo za kimataifa, diplomasia ya Tanzania nje ya nchi imeimarika.

Anasema, kuimarika siasa za nje kumeyafanya mataifa kuishika mkono Tanzania kwa kuiunga mkono katika harakati zake za kuimarisha uchumi na maendeleo.

Rais Samia alisema katika uongozi wake atahakikisha unayafikia malengo ya maendeleo endelevu yaliyowekwa na Umoja wa Mataifa (UN), huku akisisitiza mwanamke hataachwa nyuma katika safari hiyo.

Katika kuadhimisha Siku 100 za Rais Samia madarakani, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alibainisha kuongezeka miradi mipya ya uwekezaji inayosajiliwa nchini, baada ya mkuu wa nchi mpya kuimarisha uhusiano wa kimataifa.

Mnamo Juni 27, mwaka huu, kwenye ufunguzi wa kongamano la Siku 100 za Rais Samia jijini Dar es Salaam, Majaliwa alisema katika kipindi hicho cha miezi mitatu madarakani, ilisajiliwa miradi mipya 93 yenye thamani ya dola za Marekani bilioni 1.6 inayozalisha ajira 24,600 kwa vijana.

Serikali iliyoko madarakani, kupitia ilani yake ya uchaguzi iliahidi kutengeneza ajira mpya milioni nane katika miaka hiyo mitano.

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Ushiriki wa jamii unatakiwa sana katika vita biashara dawa kulevya






**NA SABATO KASIKA**
+255 783 208209

KATIKA kudhibiti biashara vya dawa za kulevya pamoja na matumizi yake, kuna mambo yanatolewa kwa Watanzania kutoa ushirikiano wa ngazi ya juu, ili kufanikisha mkakati huo wanaojihusisha na biashara hiyo.

Hapo ni ama kwa hiari au lazima, ila kuacha ni muhimu kwa hali yoyote ile. Ni wito kutoka Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) inayosema, matumizi ya dawa hizo yanaendelea kuongezeka nchini na inautaka umma wa Watanzania kushiriki katika vita hiyo.

Ni kauli nzito kutoka kwa Kamishna Jenerali wa Mamlaka hiyo, Gerald Kusaya, alipokabidhi vifaa katika kliniki ndogo ya Gereza la Segerea, Dar es Salaam hivi karibuni, kwa ajili ya kutoa matibabu kwa waraibu wa dawa za kulevya.

Anasisitiza tatizo la dawa za kulevya nchini bado ni kubwa, kwa kuwa watu wanaotumia dawa aina ya heroin wapo 500,000 na hapo hawajajumuisha wanaovuta bangi, anaowakadiria kuwa wengi zaidi.

Kusaya anafafanua zaidi kwamba. waraibu wa dawa za kulevya waliopo nchini hadi sasa ni 16,000 na wote wanaendelea kupata dawa ya methadon kila siku, huku akitoa onyo kwa wafanyabiashara wa dawa hizo kuna ‘chamotoc watakiona’.

Kamishna Jenerali huyo, anaenda mbali akinyoosha kidole kwa wanaojihusisha na biashara ya dawa za kulevya wakae chonjo, kwani wakinaswa na ushahidi, safari ya kuhamia jela maisha iko jirani nao na kwamba, wao mamlaka wenye wajibu wamejipanga kuwanasa kokote waliko, usiku na mchana.

Sasa ili kufanikisha vita hivyo vyenye maana chanya kwa kila Mtanzania, athari zake zikimhusu moja kwa moja kila Mtanzania, ni kwamba ni hali inayohitaji ushirikiano kutoka kwa kila mwananchi.

Utoaji taarifa zitakazosaidia mamlaka hiyo na nyinginezo kufanikisha vita kukabili biashara ya dawa za kulevya nchini, ni jambo muhimu.

Takwimu mbalimbali zimekuwa zikionyesha kuwa waathirika wakuu wa matumizi ya dawa za kulevya ni watoto na vijana wenye umri kuanzia miaka 15 hadi 35, ambao kimsingi ni taifa la kesho. Vijana wa aina hiyo hawawezi kuwa na manufaa kwa umma na taifa kwa ujumla, hivyo wito wa kutaka ushirikiano kwa kutoa taarifa za kusaidia kukomesha biashara ya dawa za kulevya ni muhimu.

Imekuwa ikidaiwa kuwa baadhi ya vijana wamekuwa wakitumiwa kama wakala, katika mchakato wa kukuza na kudumisha biashara na matumizi ya dawa za kulevya katika maeneo mbalimbali duniani.

Nakumbuka Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Fakharia Shomar Khamis, aliwahi kurusha tuhuma kwa watumiaji wa dawa za kulevya kuwa ndiyo wanaongoza kwa wizi wa vyuma kwa ajili ya biashara ya vyuma chakavu, ambayo inashamiri nchini.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Jenister Mhagama, akakiri kwamba vijana wengi wanaojihusisha na shughuli hiyo, wamekuwa na dalili na viashiria vya matumizi ya dawa za kulevya.

Kimsingi, serikali imekuwa na nia ya dhati katika kupambana na janga hilo, kwani linapoteza nguvukazi ya taifa ambayo ni vijana, kwa kukamata wanaojihusisha na biashara hiyo.

Ninaamini serikali pekee yake haiwezi kufanikisha vita dhidi ya ya biashara hiyo, bila ushirikiano kutoka kwa wananchi, hasa kutokana na ukweli kwamba, wahusika wake wamo ndani ya jamii.

Biashara ya dawa za kulevya imekuwa ni kikwazo cha maendeleo ya vijana katika nchi mbalimbali duniani ikiwamo Tanzania.

Wapo ambao sasa hushinda kwenye vituo vya daladala wakifanya kazi ya upigaji debe wa daladala, ili angalau wapate ujira wa Sh. 100 au 200 ambazo bado zinaishia katika kununua ‘unga’ na wamebatizwa jina la kejeli ‘mateja’.

Hivyo, ushiriki wa jamii kutoa taarifa sahihi kwa mamlaka husika, unaweza kusaidia kuokoa nguvukazi ya taifa inayoendelea kuangamia kwa matumizi ya dawa hizo.

UCHUMI

MPANGO MAENDELEO & UCHUMI BLUU...

# TAFIRI yafungulia Mwanza njia kupitia vizimba samaki Viktoria

- RC mstaafu, aliyepo waonyesha pakutokea

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

HIVI karibuni serikali ilizindua Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano kuanzia 2021/22 hadi 2025/26, ukiwa na dhima ya kujenga Uchumi Imara Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu.

Ni hatua yenye dhima ya kuchochea uchumi shindani, shirikishi na kuimarisha uzalishaji wa ndani na utoaji huduma, kukuza uwekezaji na biashara, kuchochea maendeleo ya watu na kuendeleza rasilimali watu.

Katika Mpango huo utakaogharimu Sh. trilioni 114.8, serikali itachangia Sh. trilioni 74.2, huku sekta binafsi ikichangia Sh. trilioni 40.6.

Ni mpango unaozingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025, sera na mikakati kisekta na tafiti zilizofanyika nchini, pamoja na Dira ya Afrika Mashariki ya 2050.

### KUTOKA MWANZA

Katika kuitikia jitihada hizo za kupambana na umasikini na ukosefu wa ajira, serikali mkoani Mwanza imejipanga kuwezesha miradi ya ufugaji samaki kwa vizimba ndani ya Ziwa Victoria, ili kuwawezesha wananchi kunufaika na 'uchumi wa bluu.'

Ni mradi unaolenga kutumia fursa zilizopo kwenye 'uchumi wa bluu' utakaogharimu Sh. bilioni 1.9 ili kuwasaidia vijana na kada nyinginezo kujiajiri na kunufaika kiuchumi, pamoja na kuboresha maisha ya jamii. Takwimu zinaonyesha, tangu mwaka 2016 jumla ya vizimba 109 vya ufugaji samaki vilijengwa ziwani Victoria na kwa sasa vimefikia vizimba 431 vinavyomilikiwa na wafugaji 28.

Hillary Mrosso, mtafiti mwandamizi kutoka Taasisi ya Utafiti wa Samaki Tanzania (TAFIRI), akiwasilisha taarifa yake kwenye mafunzo ya namna ya kuandaa na kuwasilisha taarifa za sayansi, teknolojia na ubunifu kwa watafiti na waandishi wa habari, anaeleza njia zilizochukuliwa.

Katika mafunzo hayo yaliyoandaliwa na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), anasema duniani kote ufugaji samaki ndio njia mbadala wa kuzalisha samaki, ili kuziba pengo litokanalo na kupungua samaki wa asili.

Mrosso anafafanua, mseto wa ufugaji samaki na kilimo ni eneo lenye fursa ya kukuza 'uchumi wa bluu' ambako uzalishaji vyanzo mbadala vya protini ya kulishia samaki, unahitaji kufanyiwa tafiti.



Mtafiti Mwandamizi kutoka TAFIRI Mwanza. Hillary Mrosso, akieleza namna maabara ya kutengeneza chakula cha samaki inavyofanya kazi. **PICHA: NEEMA EMANUEL**

> **Ili kwenda sambamba na Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano, watalaamu wa ndani watumike kuzalisha, akionya wasitumike madalali.**

Anatoa takwimu, vifaranga waliozalishwa wako 313,215 wenye bei ya wastani na kuna wafugaji 119 wamenufaika na mbegu bora ya samaki, pia wamepata mafunzo na ushauri nasaha kuhusu ufugaji bora wa samaki.

Matokeo yake ni kuongezeka uzalishaji samaki kupitia ufugaji utakaoziba pengo la upungufu wa samaki wanaovuliwa katika maji ya asili na kukua uwezo wa taasisi katika uzalishaji mbegu na vyakula bora vya samaki kwa ajili ya wafugaji.

Anasema, TAFIRI inalenga kushirikiana na wadau wa ukuzaji viumbe maji katika utekelezaji miradi katika Kanda ya Ziwa, ili kuhakikisha gharama za mradi zinachangiwa kupitia mauzo ya mbegu na vyakula vya samaki vinavyozalishwa.

### SHIDA KATIKA MABWAWA

Anazungumzia shida zinazowakabili ni kukosekana uzio katika eneo la mabwawa, kwani wamekuwa wakikabiliwa na tatizo la wezi wanaovamia maeneo hayo na kuiba samaki.

Pia, anataja miundombinu chakavu, upungufu katika maabara ya ubora wa maji na viumbe wala samaki kuvamia mabwawa watakofugia.

"Tumeomba ufadhili COSTECH wa kulikarabati jengo la utafiti wa mbegu kwa sababu nilazamani pamoja na kuboreshewa mfumo wa tanki la kusukuma maji, kwa sababu maji yanaposhuka hayaingii kwenye tanki la chini kwa asilimia 100, "anaeleza

### HATUA ZINAZOCHUKULIWA

Mrosso anataja kuanzishwa vikundi vya ufugaji samaki aina ya sato wa jinsia moja kwenye vizimba, utapunguza changamoto ya ajira kwa vijana, kuwanufaisha kiuchumi na kimazingira.

Anasema sekta ya uvuvi, ufugaji wa samaki unahitaji kutumia teknolojia ya kisasa ya vizimba ambavyo vifaranga vya samaki vinawekwa ndani ya kizimba kilichotengenezwa madhubuti kwa ama chuma au plastiki, baada ya kutumbukizwa majini.

Mtafiti huyo anaeleza vifaa hivyo vinapaswa kuwa vyepesi, visivyopata kutu, visivyo na sumu na vinastahimili mabadiliko hali ya hewa. Vilevile anafafanua, vifaa vinavyotumika kutengeneza vizimba hivyo vya maumbile tofauti ni pamoja na nyavu, mabomba, mbao, maboya, kamba na nanga.

### RC MSTAAFU ACHANGIA

Mkuu wa Mkoa wa zamani wa Dar es Salaam na Kilimanjaro, Mecky Sadiki, anatoa uzoefu wake kwenye uwekezaji wa ufugaji samaki kwa vizimba, kwamba licha ya Tanzania kumiliki asilimia 53 ya Ziwa Victoria, bado haijanufaika nao kutokana na migongano ya sheria akilinganisha na nchi jirani.

Anasema ufugaji samaki vizimbani 'unalipa' na anawashauri watu wasiogope au kukatishwa tamaa na gharama za uwekezaji, kwani kuna soko la uhakika, ikiwamo malighafi ya kutengeneza chakula cha samaki.

Anafafanua utumiaji vizimba samaki ni bora na wa kisasa, kwa sababu eneo dogo linazalisha samaki wengi na suala la gharama mwanzo wa mradi hazikwepeki.

Sadiki anachanganua mtaji ulivyo, kwamba kizimba kinagharimu Sh. milioni 20, inayohusisha vifaranga 10,000, gharama za ujenzi na vibali vyote.

Anawashauri wanaotaka kufuga samaki kwa njia hiyo, waungane kwenye vikundi na kupata nguvu ya kuanzisha kizimba kimoja kisha wataendelea kuongeza vingine kadiri watakavyokua kibiashara na kusisitiza ufugaji huo unalipa, wasiogope gharama.

### RC WA MWANZA

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mhandisi Robert Gabriel, anasema mkoa huo kwenye 'uchumi wa bluu' bado haujafanyiwa kazi ya kina, ilhali malighafi na ziwa, nguvu kazi ipo ikiwamo ya wasomi.

Anasema lengo la mpango huo wa Maendeleo wa Miaka Mitano kipindi cha kwanza, ni kutumia vizuri rasilimali za nchi, kuondokana na umasikini na tayari mpango umeshabeba dhana ya kuangalia fursa za ukuaji wa uchumi.

Pia, anashangaa chakula cha samaki kuagizwa kutoka nje ya nchi, akihoji nchi ilikokwama na anashauri wasomi waliopo waangalie mazingira ya kukuza uchumi wa Mwanza, lengo ni kunufaika na rasilimali zake, zilete mapinduzi ya kiuchumi.

Anasema, ili kwenda sambamba na Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano, watalaamu wa ndani watumike kuzalisha, akionya wasitumike madalali.

Mkuu wa mkoa anasisitiza anachokitaja 'biashara ni uchumi na nguvu ya nchi', hivyo shida zinazoibuliwa za ucheleweshaji kutoa nyaraka, nishati ya umeme na nyingine, zitafutiwe ufumbuzi ili kuweka mazingira bora uwekezaji.

Pia, anataja kubuniwe mikakati ya kuwezesha viwanda vilivyopo kuwa shindani na kuhamasisha mashirika ya umma na sekta binafsi kuwekeza katika uanzishaji wa viwanda saba vipya vya kusindika na kuongeza thamani ya mazao ya samaki.





# RC ataka kiwango kwa makandarasi wa barabara

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, amewataka makandarasi waliopewa miradi ya barabara katika mkoa huo kuifanya kwa kiwango kizuri ili waendelee kuaminiwa.

Akizungumza katika hafla ya utiaji saini mikataba ya ujenzi na matengenezo ya barabara, Mtaka alisema bajeti ya Mkoa wa Dodoma ni sawa na mikoa mitano, hivyo makandarasi hao wanatakiwa kufanya kazi ya kueleweka ili kazi nyingine inapotokea waweze kuaminiwa.

"Nawaambia makandarasi hii bajeti tuliyonayo hapa ni ya mikoa mitano kaa hapa fanya kazi ili upate kazi nyingine. Juzi nimeenda Donbosco wana eneo pale ikifika wakati wa mvua mtihani, kule Nkuhungu kuna shule inajengwa wakati wa mvua kuna shida kubwa natamani tuende kufanya miradi mizuri," alisema.

Vilevile, alisema wamesaini mkataba huo kwa upendo jambo ambalo ni jema lakini baada ya miezi mitatu hali huwa tofauti kwani upendo huo hugeuka na kuwa chuki.

"Tumekuja kwenye jambo jema kusaini sasa inaleta shida sana nyinyi mmetualika kwa upendo halafu baada ya miezi mitatu huu upendo unageuka na kuwa chuki, kesho TAKUKURU anageuka anawaweka ndani jambo hili linaniumiza.

"Tumeitana hapa baada ya miezi mitatu hali inakuwa mbaya tumekuja kushuhudia jambo jema, ndio maana makandarasi wa Tanzania hatukui kwa sababu ya ubabaishaji matarajio yangu anayefanya kazi kwa milioni 40 'focus' yake ni bilioni moja," alisema.

Aidha, Mtaka alisema kuna haja ya wafanyakazi wa serikali kuwajibu vizuri wananchi wanapokwenda ofisini kwa ajili ya kupata huduma mbalimbali.

"Hapa Dodoma anaweza akaja mtu kumbe ni ofisa mwenzako, mjibu mtu vizuri anapokuja ofisini kwako ukikubali kuwa mfanyakazi wa serikali wala usikwaze watu ndio kazi yako,"alisema.

Pia Mtaka alisema anatamani kuona makandarasi wanawake wanaongezeka katika ujenzi wa barabara na majengo.

"Ningetamani kuona makandarasi wanawake sijui tutafanyaje kwa sababu kazi zipo TANROAD yale magrupu ya whatsap tuna miradi ili watu waombe sasa wanawake wamepata wangapi katika makandarasi 29," aliesema.

Mratibu wa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) Mkoa wa Dodoma, Mhandisi Lusako Kilembe, alisema miradi yote kwa ajili ya ukarabati wa barabara katika Mkoa wa Dodoma itagharimu Sh. bilioni 48.97.

Alisema kwa Halmashauri ya Jiji la Dodoma kuna matengenezo ya barabara ya Kisasa, Itega, Njendengwa na Dodoma Mjini pamoja na uzibaji wa viraka na uwekazi wa alama za barabarani ambapo jumla ni Sh. bilioni 193.492 zitatumika.

Pia, alisema kuna matengenezo ya barabara katika maeneo ya Ndejengwa na Itega kwa kutumia teknolojia ya nguvu kazi ambapo alidai wametenga milioni 58.9 kwa ajili ya matengenezo hayo.

Vilevile, alisema kwa upande Wilaya ya Bahi zimetengwa Sh. milioni 948.264 kwa ajili ya ujenzi wa barabara za Mwitikira na Mtitaa kwa kiwango cha Changarawe.

Alisema kwa upande wa Halmashauri ya Chamwino kutakuwa na miradi mitatu ya kutengeneza barabara yenye thamani ya Sh. bilioni 3.36.

Alisema kwa upande wa Kongwa jumla ya miradi yenye thamani ya Sh. bilioni 2.09 itatekelezwa na kuna miradi ya kutengeneza barabara kwa nguvu kazi thamani yake ni milioni 40 pamoja na matengenezo ya kawaida Mtanana, Makawa kwa kutumia vikundi maalum.



Baadhi ya wakuu wa taasisi mbalimbali za kifedha nchini wakishiriki mkutano mkuu wa 20 wa taasisi hizo, ulioandaliwa na Benki Kuu ya Tanzania, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Tume ya Haki za Binadamu yataka usimamizi sheria barabarani

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TUME ya Haki za Binadamu na Utawala Bora imeishauri serikali iendelee kuboresha miundombinu ya barabara ikiwamo kusimamia sheria za barabarani kwa makini.

Aidha, imesema kwa kufanya hivyo kutasaidia kuondoa changamoto zilizoko za ukaguzi wa magari, upotevu wa haki za waathirika wa ajali, upatikanaji wa takwimu sahihi, na utaratibu wa utoaji wa adhabu kwa madereva.

Vilevile, Tume hiyo imesema serikali inapaswa kuhimiza matumizi ya teknolojia zaidi itakayowawezesha wakaguzi kufanya kazi yao ya ukaguzi wa magari kwa ufanisi na uwazi zaidi.

Hayo yalibainishwa na Makamu Mwenyekiti wa Tume za Haki za Binadamu na Utawala Bora, Mohamed Khamis Hamad, katika taarifa yake kwa vyombo vya habari kwenye Wiki ya Usalama Barabarani inayoendelea hapa nchini.

Alisema serikali iboreshe na kuongeza vituo vya ukaguzi pamoja na kuwapatia askari wa usalama barabarani vifaa vya kisasa ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi.

Alisema serikali ikizingatia matamko yanayotolewa na taasisi mbalimbali basi yatasaidia kuimarisha usalama barabarani.

Taarifa hiyo ilifafanua kuwa kamishna wa kazi asimamie matakwa ya sheria inayomtaka kila mwajiri kutoa mikataba ya ajira kwa wafanyakazi wake.

Alisema hii itasaidia kuweka mazingira bora ya kazi kwa madereva na Jeshi la Polisi na wadau wengine waendelee kutoa elimu kwa madereva na wananchi kuhusu matumizi sahihi ya barabara ili kuepusha ajali.

Aidha, alibainisha kuwa madereva na wananchi waendelee kuhimizwa kuzingatia sheria za usalama barabarani.

Kadhalika, aliongeza kuwa jamii inapaswa kuwa mstari wa mbele kutoa taarifa pale wanapoona madereva wanakwenda kinyume na sheria za barabarani na kusababisha ajali.

"Naomba wananchi mjifunze kutoa taarifa tunahitaji kuona usalama unakuwapo barabarani," alisema Hamad.

# Bahi yapokea mbegu bora za alizeti

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WILAYA ya Bahi imepokea tani 28 za mbegu bora za alizeti huku kila kata ikipatiwa tani moja kwa ajili ya kuwauzia wakulima wa zao hilo ili wafanye kilimo chenye tija na kujikwamua kiuchumi.

Hayo yalibainishwa jana na ofisa kilimo wa Kata ya Kigwe Wilaya ya Bahim, Abdallah Mdiliko, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kuinua kilimo cha alizeti.

Alisema wakulima wamechangamkia mbegu ya alizeti iliyotolewa na serikali kwa bei ya ruzuku, hali inayomaanisha kutakuwa na ongezeko kubwa la uzalishaji wa zao hilo katika Wilaya ya Bahi kama serikali ilivyokusudia kufanya kilimo hicho.

Aliema mbegu hizo zimekuwa zikiuzwa kwa bei ya ruzuku ya Sh. 7,000 kwa kilo mbili na mpaka sasa asilimia 75 ya mbegu zimeshanunuliwa na wakulima.

Alisema wamejipanga kuhakikisha wakulima wanatumia mvua zinazotarajiwa kunyesha hivi karibuni kwa kupanda mazao yanayostawi katika maeneo yao na kupanda katika maeneo yaliyotifuliwa.

Kadhalika, Mdiliko alisema mvua zimekaribia kuanza na wakulima wameanza kuberega mashamba na wengine tayari wamelima wanasubiri tu mvua zinyeshe ili wapande.

Vilevile, alisema wamekuwa wakisisitiza sana kwa wakulima, kutifua mashamba ili kufanya maji yasitembee shambani na kwenda kusababisha maporomoko.

Hata hivyo, alisema kuwa watu wengi hawalimi mpaka chini bali wanalima kwa kuparua na mvua inaponyesha maji yanapita na kuacha udongo ukiwa mkavu.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Kigwe, Jeremiah Sobayii, alisema wanaishukuru serikali kwa kutoa mbegu za ruzuku za alizeti ambalo ni zao la kimkakati hali itakayowezesha watu wa kipato cha chini kumudu bei.

Alisema kata hiyo yenye wakazi 3,900 shughuli kubwa ni kilimo na ufugaji hivyo mbegu hizo zitasaidia kuwainua wakazi wa eneo hilo.





# RC aishukia kampuni ununuzi tumbaku madai ya wakulima

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, ameijia juu kampuni ya ununuzi wa tumbaku ya MO Green International Ltd kutokana na kuchukua tumbaku ya wakulima wilayani Chunya bila kuwalipa zaidi ya Sh. milioni 460.

Ameitaka kampuni hiyo kulipa fedha hizo kabla ya Aprili, mwakani na kwamba alitaka aanze kuishughulikia sasa hivi lakini akabaini kwamba kuna makubaliano ambayo kampuni hiyo imeingia na wakulima kuwa italipa ikifika wakati huo.

Homera alionyesha kukerwa na kampuni hiyo alipofanya ziara ya kuwatembelea wakulima wa tumbaku wilayani hapa kwa ajili ya kukagua maandalizi ya msimu mpya, kukagua vitalu vya miche ya miti iliyoandaliwa na kufungua ghala la kuhifadhia tumbaku la Chama cha Msingi cha Igagwe (AMCOS).

Alisema endapo kampuni hiyo haitalipa fedha hizo ifikapo Aprili, atalichukulia hatua za kisheria kwa kuwa imesababisha hasara kwa wakulima ikiwa ni pamoja na kukwamisha kilimo cha zao hilo.

Mkuu wa mkoa alisema alishawahi kukutana na malalamiko ya wakulima wa mkoa wa Katavi alipokuwa mkuu wa mkoa huo wakiilalamikia kampuni hiyo kuwa ilichukua tumbaku yao bila kuwalipa na kwamba alifuatilia mpaka wakalipwa.

"Hawa lazima nishughulike nao. Wakitaka wakimbie nchini na hata wakifanya hivyo tutafuatilia kwenye ubalozi wao mpaka fedha hizo zote zilipwe. Nawaomba wakulima endeleeni kuvuta subira mpaka mwezi huo ambao viongozi wamekubaliana halafu wasilipe waone," alisema Homera.

Aliitaka Bodi ya Tumbaku Tanzania kuhakikisha inawapelekea wakulima wa tumbaku wanunuzi wa uhakika kwa kufuatilia historia yao kuanzia nchi wanakotoka na uzoefu wao kwenye ununuzi wa zao hilo kwenye mataifa mengine.

Awali, Ofisa Ushirika kutoka Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, Mkoa wa Mbeya, Biezery Malila, alisema mbali na kampuni hiyo kudaiwa na wakulima pia inadaiwa ushuru na Chama Kikuu cha Ushirika wa Wakulima wa Tumbaku (CHUTCU) pamoja na vyama vya msingi.

Alisema mpaka sasa kampuni hiyo inadaiwa Dola za Kimarekani 39,660.21 ambazo ni za vyama vya msingi vya Kalangali, Nkung'ungu, Malangali, Mapinduzi pamoja na CHUTCU.

Kitendo cha kampuni hiyo kuchelewa kuwalipa wakulima hao, alisema kimekuwa na athari kwa wakulima ikiwamo kushindwa kuandaa mashamba kwa ajili ya msimu wa kilimo ujao kutokana na kutokuwa na fedha za kuwalipa vibarua.

Pia alisema baadhi ya wakulima wameshindwa kuwapeleka watoto wao shule kutokana na kukosa fedha kwa ajili ya ada na kwamba wengine wameshindwa kulipa madeni waliyokuwa wanadaiwa wakati wa kuandaa mashamba msimu uliopita.

Alisema tatizo hilo limesababisha vyama vya msingi kushindwa kujiendesha kwa kushindwa kuwalipa wafanyakazi ambao vimewaajiri kwenye ofisi zao.

"Baada ya kuona tatizo hili limekuwa kubwa tuliamua kumshirikisha Mkuu wa Wilaya ambaye ametusaidia mpaka sasa kampuni hiyo imeshawalipa wakulima Dola 907,515.50 kati ya Dola milioni 1.16 na baada ya kulipa fedha hizo ndipo waliahidi kumalizia mwezi Aprili," alisema Malila.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Simon, alisema ofisi yake imekuwa ikishirikiana na wakulima kufuatilia fedha hizo na kwamba alibaini kuwa kampuni hiyo haina mtaji wa kutosha kufanya biashara ya tumbaku.

Alisema ili kuondokana na tatizo hilo Bodi ya Tumbaku inatakiwa kufuatilia kwa kina kampuni zinazonunua tumbaku ili kuepuka migogoro isiyokuwa ya msingi kwa madai kuwa mpaka sasa kuna migogoro kati ya wakulima na viongozi wa vyama vyao vya msingi.

## Wananchi walia ubovu barabara

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

WANANCHI wa vijiji vya Kyobo Juu na Kyobo Chini vilivyoko Kata ya Ikuti wilayani Rungwe wameiomba serikali kuwasaidia kujenga barabara yao waliyoilima kwa mkono miaka mingi iliyopita ili magari yaweze kupita.

Wakizungumza juzi na Nipashe, wananchi hao walisema kuwa barabara pekee inayoingia kwenye vijiji hivyo waliilima wenyewe kwa mikono miaka mingi iliyopita na haijawai kulimwa.

Deus Mwaijumba alisema kwa namna barabara hiyo ilivyolimwa na wazee wao miaka mingi iliyopita, magari hayawezi kupita na kuvifikia vijiji vyao, hivyo wanaomba msaada wa serikali iiboreshe ili iweze kupitika.

"Barabara hii ambayo ndiyo inaingia kwenye vijiji vyetu vya Kyobo Juu na Kyobo Chini haijawahi kutumiwa na magari tangu nchi ipate uhuru. Hii ni kwa sababu ililimwa kienyeji na wazee wetu kwa kutumia jembe la mkono miaka mingi iliyopita, tunaomba sasa serikali itusaidie kuilima kwa greda ili magari yapite na kufika kwenye vijiji vyetu," alisema Mwaijumba.

Alisema katika vijiji hivyo wanazalisha mazao mengi ya biashara na chakula kama vile ndizi, iliki, kahawa, magimbi na mihogo lakini hawawezi kuyasafirisha kwa wingi kwenda kuyauza.

Naye Lucia James alisema kuwa ukosefu wa barabara pia unaathari kubwa kwa wanawake hasa wajawazito wanapohitaji kujifungua pale wanapotaka kwenda kwenye vituo vya afya.

Alisema usafiri pekee unaowasaidia wanawake wajawazito kwenda kujifungua kwenye vituo vya afya ni pikipiki, usafiri aliodai kuwa sio rafiki kwa baadhi ya wajawazito hasa ambao wanakuwa na matatizo ya uzazi.

"Baadhi ya wajawazito wanajifungulia njiani wakati wakienda kwenye kituo cha afya kutokana na kukosekana kwa usafiri wa gari, pikipiki ndio zinatusaidia lakini kwa baadhi ya wanawake haziwafai na wengine wanajikuta wanapoteza watoto kwa kukosa huduma," alisema Lucia.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Mpokigwa Mwankuga, aliungana na wananchi hao kuomba msaada wa ujenzi wa barabara hiyo, akisema kuwa Serikali Kuu inapaswa kutenga bajeti ya kuwasaidia wananchi hao katika mwaka ujao wa fedha.



Naibu Spika Dk. Tulia Ackson (watatu kushoto), akiongoza matembezi ya hisani jijini Mbeya juzi, yaliyokuwa na lengo la kukusanya fedha kwa ajili ya kutunisha Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti Ukimwi nchini (ATF), ambapo zaidi ya Sh. milioni 130 zilipatikana. Wapili kushoto ni Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya kudhibiti Ukimwi (TACAIDS), Dk. Leonard Maboko. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wazazi wahimizwa kuwalinda watoto na vitendo vya ukatili

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAZAZI na walezi mkoani Mbeya wameshauriwa kuwalinda watoto wao dhidi ya vitendo vya ukatili hasa ubakaji na ulawiti bila kujali jinsia zao kwa kuwa watoto wa jinsia zote wako katika hatari ya kufanyiwa ukatili.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Mkoa wa Mbeya, Stella Kategile, aliyasema hayo juzi jijini hapa wakati wa Usiku wa Mkono wa Mama Gala na Paradise Mission uliofanyika kwa lengo la kuwapatia mafunzo mbalimbali wanawake wa mkoa huo.

Kategile alisema zamani wazazi na walezi walikuwa wanahamasishwa kuwalinda zaidi watoto wa kike kutokana na kwamba walikuwa wanakumbwa zaidi na vitendo vya ubakaji lakini kwa sasa vitendo vya ulawiti kwa watoto wa kiume vimekithiri. Alisema kutokana na tatizo hilo, wazazi wanatakiwa kuwalinda watoto wote kwa kuhakikisha wanacheza na kushinda kwenye mazingira ambayo watakuwa salama dhidi ya vitendo hivyo.

Alisema katika Mkoa wa Mbeya, wanawake wengi wanajituma kufanya kazi za kujitafutia kipato hali ambayo wakati mwingine inaweza kusababisha wakashindwa kuwalinda watoto wao, hivyo wakakumbwa na vitendo vya ukatili.

"Ni kweli tunatakiwa kutafuta kipato, lakini ninachowaomba wanawake wenzangu ni kuhakikisha mnawalinda watoto, siyo wewe unaondoka asubuhi na kurudi usiku bila kujua watoto wako wameshinda wapi na walikuwa na nani, siku hizi kuna watu wanaiba watoto," alisema Kategile.

Aliwapongeza wanawake hao ambao ni wanachama wa Mkono wa Mama Gala kwa kusaidia kwenye malezi ya watoto ikiwa ni pamoja na kuwasomesha kwenye ngazi mbalimbali za elimu watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu.

Awali, Mkurugenzi wa Taasisi ya Mkono wa Mama Ghala, Olime Mwakilembe, alisema taasisi hiyo kwa sasa ina wanachama 100 na kwamba inalenga kutoa huduma mbalimbali kwa jamii ikiwamo kuwahamasisha wanawake kufanya kazi.

Taasisi hiyo, alisema imekuwa ikiwasaidia wanawake mitaji kwa ajili ya kufanya biashara mbalimbali na kwamba mpaka sasa imewasaidia zaidi ya wanawake 80 kupata mitaji ya biashara na kwamba huwa wanawatembelea kwa ajili ya kuangalia maendeleo ya shughuli zao.

Pia alisema taasisi hiyo imekuwa ikisomesha watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu na kwamba mpaka sasa imesomesha watoto watano katika ngazi mbalimbali na kwamba mpaka sasa inaendelea kuwasomesha baadhi.

"Ili kuimarisha shughuli zetu za kujiongezea kipato, tuna mpango wa kununua mashine ya kukamua mafuta ya aliseti ambayo itagharimu Sh. milioni 16, hivyo tunawaomba wadau mbalimbali watusaidie ili tufanikishe ndoto yetu hiyo," alisema Mwakilembe. Alisema kwa sasa taasisi hiyo imekuwa ikilelewa na Mkurugenzi wa Shule ya Paradise Pre and Primary School iliyopo katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi, Ndele Mwaselela.

Mwakilishi wa Shule ya Paradise Mission, Aikande Lema, ambaye ni mwanasheria, alisema watoto wote wana haki sawa kwa mujibu wa sheria za nchi na kwamba wanastahili haki sawa ikiwamo kwenye urithi wa mali za wazazi.



# Kiwango ukosefu ajira chazidi kupaa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema kiwango cha ukosefu wa ajira kwa vijana kimeongezeka kutoka asilimia 12.1 mwaka 2014 hadi kufikia asilimia 12.6 mwaka 2021/21.

Amesema kutokana na hali hiyo, kuna haja ya kuwapo uimarishaji wa sera na mikakati mbalimbali kukabiliana na tatizo hilo.

Majaliwa aliyasema hayo juzi alipokuwa akizindua matokeo ya viashiria muhimu vya soka la ajira kutokana na utafiti wa watu wenye uwezo wa kufanya kazi wa mwaka 2020/21 katika Hoteli ya Golden Tulip, Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Amani Abeid Karume.

Pamoja na juhudi kubwa zinazofanywa na serikali kukabiliana na changamoto hiyo ya ukosefu wa ajira, alisema bado kuna vijana wenye umri wa miaka 15 hadi 35 kutokuwa na ajira.

Alisema ukosefu wa ajira kwa wanawake ni asilimia 12.7 ikilinganishwa na wanaume ambao ni asilimia 5.8.

Kwa upande wa Zanzibar, alisema kiwango cha ukosefu wa ajira kimeongezeka kidogo kutoka asilimia 17.4 mwaka 2014 na kufikia asilimia 19.7 mwaka 2021 wakati upande wa Tanzania Bara kimepungua kidogo kutoka asilimia 10.3 mwaka 2014 na kufikia asilimia 9.0 mwaka 2020/21.

Alisema matokeo ya utafiti uliofanyika yanaonyesha kuwa taifa lina ongezeko la nguvu kazi ya watu milioni 3.7 katika kipindi cha miaka sita iliyopita kutoka watu milioni 22.9 mwaka 2014 hadi watu milioni 26.6 mwaka 2020/21.

Pia alisema idadi ya watu walio na ajira imeongezeka kutoka watu milioni 20.5 mwaka 2014 hadi watu milioni 24.1 mwaka 2020/21 sawa na ongezeko la asilimia 17.5. Kati ya hao, alisema wanaume ni milioni 12.4 (sawa na asilimia 51.4) na wanawake ni milioni 11.7 sawa na asilimia 48.6.

Alisema katika kukabiliana na hali hiyo, serikali itahakikisha inaongeza kasi ya kuweka mazingira mazuri ya biashara na uwekezaji, utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali zenye lengo la kuwezesha nguvu kazi kuajiriwa na kujiajiri.

Naye Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, alisema Serikali ya Zanzibar itaendelea kutoa ushirikiano ili kuhakikisha utafiti huo unafanyiwa kazi kwa ajili ya maendeleo ya pande zote za Muungano.

Alisema, utafiti huo una viashiria vingi muhimu vinavyohusiana na masuala ya ajira, hivyo serikali itaendelea kuchambua viashiria vyote na kuhakikisha inaandaa na kutekeleza programu za pamoja za kukuza ajira kwa wananchi wake.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Jenister Mhagama, alitaka kuwapo vipaumbele kwa vijana waliohitimu masomo ya fani mbalimbali katika masoko ya ajira ili kukabiliana na tatizo hilo.

Alisema Tanzania ina vijana wengi wenye elimu na hawana kazi, hivyo, tafiti hizo zitasaidia kutafuta mbinu za kukabiliana nazo kwa maendeleo ya taifa.

## Zanzibar kushirikiana na Hospitali ya India

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya, Ustawi wa Jamii Wazee, Jinsia na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui, amesema wizara yake inatarajia kushirikiana na Hospitali ya Pushpawati Singhania iliyoko New Delhi, India katika kuwapatia matibabu bora wananchi wa Zanzibar.

Alisema hayo ofisini kwake Mnazi Mmoja Mjini Unguja jana alipokutana na uongozi wa hospitali hiyo uliofika wizarani hapo kwa ajili ya kujitambulisha.

Mazrui alisema hospitali hiyo itasaidia katika kuwapatia wananchi huduma mbalimbali za matibabu yakiwamo ya moyo, matatizo ya haja ndogo na upandikizaji wa figo.

Kwa mujibu wa waziri, hospitali hiyo imeamua kwa makusudi kushirikiana na Zanzibar katika huduma za afya ili kuwasaidia madaktari wa Zanzibar kupata ujuzi na uzoefu wa kutumia mashine za kisasa na kufanya uchunguzi wa maradhi mbalimbali ya binadamu.

Pia alisema hatua inayofuata ni kuandaa taratibu za kutia saini hati ya makubaliano baina ya wizara na hospitali hiyo kwa lengo la kuanza kusaidia huduma za matibabu nchini.

Naye Meneja wa Masoko ya Kimataifa wa Hospitali hiyo, Sanoj Kumar, alisema iko haja ya kuwaleta wataalamu wao Zanzibar ili kusaidia utoaji wa huduma za matibabu kwa wananchi.

Ushirikiano huo, alisema pia utasaidia katika kupunguza gharama za matibabu kwa wagonjwa wanaokwenda nchini India kwa ajili ya matibabu.

Alisema Hospitali ya Pushpawati Singhania, itaendelea kushirikiana kwa karibu na serikali ili kuhakikisha huduma bora za afya zinapatikana Zanzibar.




Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto Zanzibar, Nassor Mazrui (kushoto), akimkabidhi kitabu cha kumbukumbu ya Zanzibar, Meneja wa Masoko ya Kimataifa wa Hospitali ya Pushpawati ya nchini India, Sanoj Kumar, alipofika ofisini kwake jana, kwa ajili ya kujitambulisha. Kulia ni mjumbe kutoka hospitali hiyo, Ratnesh Sinha. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Asisitiza umuhimu viongozi kulinda SUK

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema viongozi katika ngazi mbalimbali nchini wana wajibu wa kuitunza Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa kuwa ndio mustakabali wa ujenzi wa nchi.

Othman aliyasema hayo jana katika ukumbi wa Makonyo, Wawi Kisiwani Pemba alipozungumza na watendaji mbalimbali katika majumuisho ya ziara yake ya kukagua athari za mazingira na utoaji wa huduma za afya kisiwani Pemba.

Alisema kuwapo kwa mfumo wa serikali hiyo Zanzibar, viongozi hawapaswi kulichukulia kwamba ni jambo la kisiasa pekee na kwamba wote wana wajibu wa kuisimamia kwa nia ya kuimarisha amani na utulivu, hivyo kuharakisha maendeleo.

Kwa mujibu wa Othman, kuwapo kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar ni jambo muhimu katika kuweka ustawi wa amani ya kweli, hivyo kuwavutia wawekezaji na wahisani mbalimbali kuchangia kukuza uchumi na kuimarisha maendeleo ya Zanzibar.

Alisema viongozi na wananchi wote ni lazima watambue kwamba hivi sasa mahitaji makubwa ya nchi ni kusonga mbele kiuchumi na kijamii na kwamba uamuzi wa kuwapo SUK umepiganiwa na kuridhiwa na viongozi wote wakuu jambo lililoweka uzalendo mbele, halina budi kuungwa mkoni na kila mmoja miongoni mwa wanajamii.

Pia alisema hivi sasa kazi kubwa ya serikali ni kuwatumikia wananchi kwa kutengeneza mfumo sahihi unaotoa fursa na haki bila kuwapo ubaguzi wa aina yoyote.

Kuhusu uhaba wa wafanyakazi katika sekta mbalimbali hasa ya afya kisiwani Pemba, alisema jambo hilo limechangiwa na mtindo wa baadhi baadhi ya watumishi wanaoajiriwa kisiwani humo na muda mfupi baadaye kuomba kwenda kuendelea na kazi katika kisiwa cha Unguja.

Aliwataka viongozi mbalimbali kisiwani Pemba kutoridhia kuendelea kwa hali hiyo kwa kuwa kunachangia kudhoofisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi hasa katika sekta ya afya ambayo ndiyo uhai wa mwanadamu.

Akizungumzia suala la mazingira, Othman aliwataka wananchi kutambua kwamba jambo hilo linamuhusu kila mmoja na kuikumbusha jamii kutambuaa kwamba kila mtu anahusika na anapaswa kushiriki katika kulinda na kuhifadhi mazingira ili yasiendelea kuharibika.

Othman aliwataka viongozi na wananchi kutafakari kwa pamoja mbinu bora zaidi ya kukabili janga la kimazingira hasa kwa kuzingatia kwamba ardhi ya Zanzibar inaendelea kuliwa na bahari na kuendelea kusababisha madhara makubwa ya kimazingira.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO MJINI ILIYOPO MOROGORO

**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**

SHAURI LA MADAI NAMBA 195/2021

MDAI: EL JEHOVAH NGASA (HAMIS MDEE)

DHIDI YA

MDAIWA: ESTER ZERA MSUYA

KWA: ESTER ZERA MSUYA

OMBI LA MDAI EL JEHOVAH NGASA (HAMIS MDEE)
MADAI: Pesa sh. 500,000/=

Unatakiwa kuhudhuria hapa Mahakamani katika shauri tajwa hapo juu bila kukosa. Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 14 Mwezi 12 Mwaka 2021 saa 8:30 Asubuhi

Angalia kama *hukuhudhuria/ hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu. Mahakama ikithibitisha kama umepokea/ mmepokea kuitwa shaurini, hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/ mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii Leo tarehe 19 Mwezi 11 Mwaka 2021

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

116588102

## TANGAZO LA KUFUNGA KAMPUNI

**EMPOWERED LIFE SOLUTIONS COMPANY LIMITED.** Uongozi na wamiliki wa **EMPOWERED LIFE SOLUTIONS COMPANY LIMITED** yenye namba ya usajili **151922953,** iliyopo Masaki, Haile Selassie Road Plot No. 464 iliyosajiliwa mwaka 2021 umeamua kufunga Kampuni hiyo.

116588202

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ANDREW ANJAWE MAKWETA**

Anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba ya usajili **T 210 DDK.** Gari aina ya BREVIS. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi . Taarifa ya polisi **DOD/DOD/RB/558843/2021.**

116588502

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**ABDALLAH ABDALLAH MUSSA** anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 600 CZE – BOXER BM 125-X.** Chassis namba **MD2B15BX0MWC99549.** Engine namba JVXWMB42737.Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/CEN/RB/544600/2021.**

116588802

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**NDUGU GIDEON JORAM LYIMO** wa Dodoma anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC131 CBZ** aina ya **BOXER BM 150** yenye Chasis No. **MD2A21BY1JWB92953,** Engine No. **PFZWJB14624.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi namba **DOD/TR/RB/1888/2021**

116589202

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA MWANZO KAWE

(S.M.M 1984 NYONGEZA)
YA 5 KANUNI 2
Katika Mahakama ya mwanzo KAWE

Usimamizi wa mirathi NA. 320/2021 M.I.T 57/2021

Ombi la NEVILLE MATERU VICTOR kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu GETRUDE NYAMBO VICTOR

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA NA MIRATHI HII POPOTE ALIPO**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnano tarehe 03-12-2021 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. GETRUDE NYAMBO VICTOR.
Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.

SAHIHI YA HAKIMU

116589002

BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA TUNDURU
MAHALI TUNDURU

MAOMBI NO. 15/2021

HASHIMU SAIDI FAMBO....................MUOMBAJI

DHIDI YA

ASUNI ISSA NJADI............MJIBU MAOMBI

WITO/KUITWA SHAURINI

KWA: ASUNI ISSA NJADI – WA MAKOTENI TUNDURU

Fahamu kwamba shauri hili limepangwa kusikilizwa tarehe 14 Mwezi wa 12 Mwaka 2021 saa 2:00 asubuhi mbele ya Mheshimiwa MH: N. LUKEHA Mwenyekiti wa Baraza. Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na muhuri wa Baraza hii leo tarehe 25 Mwezi wa 11 Mwaka 2021.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
TUNDURU

116589102

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
KANDA YA DAR ES SALAAM

SHAURI LA MADAI NA. 268 YA 2021

(1) DEOGRATOUS JOSEPH MARANDU
(2) SAJIRA JUMA MMBAGA.............................WAOMBAJI

DHIDI YA

1. TALKTEL COMPANY LIMITED
2. 4G MOBILE COMPANY LIMITED
3. KISIA OMAR ALMASI...........................MJIBU MAOMBI

KWA: TALKTEL COMPANY LIMITED, 4G MOBILE COMPANY LIMITED NA KISIA OMAR ALMASI
DAR ES SALAAM.

**KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa wadai tajwa hapo juu wamefungua maombi ya gharama za kesi dhidi yako, unatakiwa kufika katika Mahakama hii tukufu wewe mwenyewe au Wakili au Mwakilishi wako anayetambulika kisheria tarehe 14/12/2021 saa 4:00 asubuhi kujibu madai dhidi yako. Unatakiwa kuleta vielelezo vyote ambavyo unatarajia kuvitumia katika utetezi wako siku hiyo.
Angalizo: Kama usipohudhuria siku iliyotajwa hapo juu, na Mahakama ikithibitisha kuwa umepokea wito huu, shauri hili litasikilizwa na kutolewa maamuzi bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa mkono wangu na chapa ya Mahakama leo tarehe 25 Novemba, 2021.

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
KANDA YA DAR ES SALAAM

116588902

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA MWANGA

UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI

SHAURI LA MIRATHI NA 3 YA MWAKA 2021

MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA
LINUS VALENTINO NZEMA............... MAREHEMU
LUCIA DANIEL MKEPULE...............MWOMBAJI

**TAARIFA YA KAWAIDA**
(Kanuni ya 75)

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua za usimamizi wa mirathi kwa muombaji aliyeomba hapo juu. Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 7 mwezi wa Desemba, 2021.

Imewasilishwa Mwanga leo tarehe 24 mwezi wa Novemba, 2021.

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA WILAYA MWANGA

116589402

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**LUCKSON DICKSON LUSWEMA** anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 688 CRA.** Kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 898 CJW.** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa za polisi: **IRI/IRI/RB/557553/2021** na **IRI/IRI/RB/557555/2021.**

116589602

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**VICTOR PANGAMAHUTE** KALINGA anatangaza kupotea kwa kadi ya Bajaji yenye namba za usajili **MC 737 CVK.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **IRI/IRI/RB/552716/2021.**

116589502

*NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA*

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

**OFISI ZA MATANGAZO**

Mikocheni Industial Area,

Po.Box 31042, Dar es Salaam. Mob: +255 - 745 700 710.

E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KITAIFA




Mkurugenzi wa Masoko wa Shirika la Bima ya Taifa (NIC), Yesaya Mwakifulefule (kushoto), akijadiliana jambo na baadhi ya wafanyakazi wa shirika hilo, waliopo katika maonyesho ya wiki ya nenda kwa usalama barabarani, kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, jijini Arusha jana. Kulia ni Meneja wa NIC Mkoa wa Arusha, John Mdenye. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# AfDB yaipa Tanzania mkopo nafuu bil. 268/-

**Na Josephine Majura**

TANZANIA imesaini makubaliano ya mkopo wenye masharti nafuu wa thamani ya dola za Marekani milioni 116.34 (takribani Sh. bilioni 268.18) kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya kutoka Mnivata-Newala-Masasi mkoani Mtwara yenye urefu wa kilomita 160 kwa kiwango cha lami.

Mkataba wa msaada huo ulisainiwa jana jijini Dar es Salaam na Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba kwa niaba ya Serikali ya Tanzania na Naibu Mkurugenzi Mkuu wa AfDB, Kanda ya Mashariki, Dk. Abdul Kamara.

Tutuba alisema kusainiwa kwa mkataba huu utaongeza kiasi cha fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi inayoendelea kutekelezwa na Serikali kupitia ufadhili wa AfDB takribani dola za Marekani bilioni 2.27 hadi kufikia dola za Marekani bilioni 2.39.

"Hiki ni kiashiria tosha cha ushirikiano mzuri na wa muda mrefu wa maendeleo tangu mwaka 1971 kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Benki ya Maendeleo ya Afrika", alisisitiza.

Alieleza kuwa fedha hizo pia zitatumika kujenga daraja la mto Mwiti lenye urefu wa mita 84, ujenzi wa stendi mpya za mabasi katika wilaya za Tandahimba, Newala na Masasi zinazonufaika na mradi, ununuzi wa magari mawili ya kubebea wagonjwa na mashine mbili za X-ray za kupima wagonjwa na utekelezaji wa mikakati ya usalama barabarani pamoja na mafunzo ya ujasiriamali kwa wanawake na vijana.

Aisema kuwa gharama za utekelezaji wa mradi ni dola za Marekani milioni 119.65 ambapo AfDB imetoa dola za Marekani milioni 116.34 na Serikali ya Tanzania itachangia dola za Marekani milioni 3.31.

Aliongeza kuwa utekelezaji wa mradi huo unalenga kuimarisha miundombinu ya usafirishaji katika Ushoroba wa Maendeleo wa Mtwara ili kuchochea kasi ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii na kupunguza umaskini kwa wananchi.

Naibu Mkurugenzi Mkuu wa AfDB Kanda ya Mashariki Dk. Kamara, alisema kuwa kukamilika kwa ujenzi wa barabara hiyo kutawezesha kuendeleza maeneo ya vijijini kwenye Ukanda huo wa Maendeleo wa Mtwara na kufanya eneo lote la barabara ya lami kufikia kilometa 816 hivyo kuchochea maendeleo ya maeneo hayo ikiwemo Bandari za Mtwara na Mbamba Bay katika Ziwa Nyasa.

"Mradi huo utarahisisha usafirishaji wa abiria na mizigo katika ukanda wa Afrika na nchi jirani ya Msumbiji, Malawi na Zambia ambazo zitahudumiwa na Bandari ya Mtawara," alisisitiza Dkt. Kamara.

## Waziri aagiza sanduku la maoni kila wizara

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya (Rais Menejimenti, Utumishi na Utawala Bora), Mohamed Mchengerwa, ameiagiza TAKUKURU kuandaa sanduku la maoni na kuweka kwenye kila wizara na taasisi zote serikali, ili kutoa fursa kwa wananchi na watumishi kuwabaini wala rushwa.

Aidha, majalada 1,053 ya kesi mbalimbali yamefanikiwa kuchunguzwa huku mengine yakiwasilishwa mahakamni kwa ajili ya kutolewa uamuzi.

Akizugumza kwenye Mkutano mkuu wa mwaka wa TAKUKURU wa kutathmini utendaji kazi wao, alisema lengo la kuanzisha masanduku hayo ni pamoja na kutoa nafasi kwa watumishi na wananchi wanaohitaji huduma wanapoombwa rushwa waweze kusema.

Alisema kumekuwa na tabia ya watumishi kutaka rushwa ili kuwahudumia wananchi wakati vitendo hivyo havikubaliki, ndio maana nimeagiza kuanzishwa kwa masanduku hayo katika taasisi na Wizara.

"Naomba suala hili likafanyiwe kazi tunahitaji kuona jamii inapata huduma kutoka kwa watuishi bia ya bugudha yoyote,"alisema Mchengerwa.

Alisema viongozi wengi hawatambui ya kuwa nchi ni ya wananchi wenyewe, hivyo TAKUKURU ina nafasi kubwa ya kuhakikisha inapambana na viongozi ambao siyo waaminifu ili kuwabaini wala rushwa.

Awali, Mkurugenzi mkuu wa TAKUKURU, Kamishina wa Polisi, Salum Hamduni, alisema hadi sasa taasisi imeshinda kesi za rushwa 345 na kushindwa kesi 156 huku ikiokoa Sh. billion 29.3.

Alisema katika kipindi cha mwaka mmoja jumla ya majalada 1,053 yalichunguzwa na kukamilika ambapo 339 yaliwasilishwa kwa Mkurugenzi wa Mashitaka (DPP) kwa ajili ya kuomba kibali cha kuwafikisha mahakamani huku kesi mpya 542 zilifunguliwa katika Mahakama mbalimbali.

## Chongolo akumbuka mabalozi nyumba 10

**Na Beatrice Shayo**

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi, Daniel Chongolo, amesema kuongezeka kwa wahamiaji haramu kumechangiwa na kuondolewa kwa mfumo wa mabalozi wa nyumba 10, ambao ulisaidia kuwatambua wageni wanapoingia hapa nchini.

Chongolo aliyasema hayo jana wakati wa majumuisho ya ziara ya sekretarieti ya chama hicho inayofuatilia utekelezaji wa ilani ya CCM katika Mkoa wa Katavi

Alisema hali siyo nzuri kutokana na wimbi la wahamiaji haramu linaongezeka nchini, jambo ambalo linahitaji kamati za ulinzi na usalama kwa kila wilaya na mikoa kufanyakazi ya kudhibiti wimbi hilo.

Alisema zamani ilifanikiwa kudhibiti wageni kutoingia ovyo katika maeneo ya makazi na vijiji kutokana na kutumia mfumo wa mabalozi wa nyumba kumi ambao sasa ameondolewa.

Alisema mfumo huo uliisaidia serikali baada ya wananchi kutoa taarifa kwa watu wasiowajua katika maeneo yao jambo ambalo kuondoa wahamiaji haramu.

Aidha alisema hivi sasa kumekuwa na migogoro msingi ya ardhi inayo sababishwa na wahamiaji haramu ambao wanahamia mapori ya hifadhi jambo ambalo linaitwisha mzigo serikali kutumia muda mwingi kutatua matatizo hayo.

Chongolo alisema kamati za ulinzi na salama katika mikoa na wilaya zinapaswa kuwa makini kwenye maeneo wanayoyasimamia kwakuwa baadhi ya wahamiaji haramu wanajifanya ni Watanzania wa kuzaliwa.

Aliongeza: "Mwaka wa pili mtu huyu anajuana na watu wa vijijini anachora ramani mwaka wa nne anakwenda kuchukua mafunzo ya ufundi na wanapenda sana fundi charahani akitoka hapo akikushonea suti utadhani imechongwa, kisha hapo anahama kesho yupo Dodoma wiki ijayo yupo Mogogoro anaimalizia Dar es Salaam unamuuliza we nani anakujibu mimi wa kabila fulani huo ndiyo ujanja wanaoutumia."

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI KISUTU**
**DAR ES SALAAM**

**KESI YA "MADAI" NA.263 YA MWAKA 2019**

**M.M.INDUSTRIES LIMITED.................................................MDAI**

**DHIDI YA**

**GREAT LAKES CONSTRUCTION...........................................MDAIWA**

**KWA:**

**MANAGING DIRECTOR,**
**GREAT LAKES CONSTRUCTION LTD: POPOTE ULIPO**

**KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa mdai ameleta madai yake ambayo maelezo ya mdai yameelezwa katika nakala ya madai ambazo zinaweza kupatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo Unahitajiwa kuhudhuria katika Mahakama hii binafsi, Wakili wako au mwakilishi wako ambaye anaruhusiwa kisheria, siku ya tarehe **16/12/2021 saa 05:00 Asubuhi,** kusomewa **maamuzi.** Mbele ya Mheshimiwa, **A. MMBANDO -PRM**

**ANGALIA:**

Kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikithibitisha kama umepokea kuitwa shaurini, itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe **22/11/2021.**

RESIDENT MAGISTRATES COURT KISUTU - DAR ES SALAAM

**HAKIMU MKAZI MKUU**
**KISUTU -DAR ES SALAAM**

216589302

# KILI MARATHON KASKAZINI WAKUMBUSHWA KUJISAJILI

**Na Mwandishi Wetu**

WENYEJI wa mbio maarufu za Kilimanjaro Premium Lager Marathon kutoka mikoa ya Kanda ya Kaskazini, ambazo mwaka huu zinatimiza miaka 20 tangu kuanzishwa kwake wametakiwa kujitokeza kwa wingi kujisajili mapema ili kuepuka usumbufu dakika za mwisho.

**Mbio za Kilimanjaro zinatarajiwa kufanyika Februari 27, mwakani katika Chuo Kikuu Cha Ushirika Moshi, mkoani Kilimanjaro na huandaliwa na Kampuni ya Executive Solutions ya hapa nchini.**

Wito huo umetolewa kutokana na uzoefu wa miaka ya nyuma ambapo washiriki kutoka kanda hiyo wamekuwa wakisubiri hadi dakika za mwisho ili kujiandikisha jambo ambalo huwaacha baadhi yao na masikitiko ya kukosa namba.

"Tunatoa wito kwa washiriki kutoka Kilimanjaro, Arusha, Tanga na Manyara kujisajili kwa njia ya mtandao kupitia www.kilimanjaromarathon.com au kwa njia ya Tigopesa kwa kupiga *149*20#," alisema Aggrey Marealle ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Executive Solutions, waratibu wa mbio hizo kitaifa.

Marealle alisema mbio hizo za mwakani zinategemewa kuwa kubwa zaidi kwa sababu itakuwa ni mwaka wa 20 tangu kuanzishwa kwake kwa hivyo washiriki wana kila sababu ya kuhakikisha wanathibitisha ushiriki wao.

"Huwa inasikitisha sana kuona washiriki kutoka Moshi au Arusha wanakosa namba wakati wanatokea katika kanda mwenyeji wa mbio hizi. Namba zikishaisha usajili huwa unafungwa. Kwa kawaida hakuna namba zinazouzwa katika vituo vya kutolea namba isipokuwa tu kwa mbio za kilomita tano kama zitakuwa zimebakia," alisema Marealle.

Aliongeza kujisajili ni rahisi mno na kwa sasa kuna punguzo la bei la asilimia 20 lakini kuanzia Januari 7, mwakani ada za usajili zitapanda. Mkurugenzi wa mbio hizo, John Bayo alisema washiriki wote wa mbio za Kilimanjaro Premium Lager (kilomita 42, Tigo (kilomita 21) na Grand Malt ambazo zitakuwa za kilomita tano wanatakiwa waanze mazoezi mapema ili kujiweka tayari na mbio hizi za miaka 20 ambazo ni za kihistoria.

"Tunataka mbio hizi ziwe za ushindani zaidi na ziache kumbukumbu ya aina yake miongoni mwa washiriki kwa hivyo maandalizi ni muhimu sana. Ni matumaini yetu zawadi nyingi zitabaki hapa nyumbani safari hii. Kama waandaaji tutafanya sehemu yetu na tunatoa wito kwa washiriki wafuate maelekezo ili kufanya mbio za mwakani ziwe za kufana zaidi, tunatarajia washiriki kutoka nchi zaidi ya 55 na umati unatarajiwa kuwa mkubwa zaidi kuliko miaka ya nyuma," Marealle alisema.

Katibu Mkuu wa Riadha Tanzania (RT), Jackson Ndaweka, alisema wameridhishwa na taarifa za maandalizi wanazopokea kutoka kwa waandaaji.

"Hili ndio tukio kubwa kabisa la riadha nchini ambalo huwaleta pamoja zaidi ya washiriki 12,000 kutoka ndani na nje ya Tanzania, kwa maana hiyo tunashirikiana na waandaaji kwa karibu kuhakikisha mbio hizi zinafanikiwa na zinaiweka riadha ya Tanzania katika kiwango cha kimataifa. Wanariadha wa hapa nchini hujipatia kipato kwa kushiriki mbio hizi, lakini pia huwandaa vizuri kuelekea mashindano ya nje ya nchi. Mbio hizi pia zinachangia kwa kiasi kikubwa katika pato la nchi kwa sababu ya watalii ambao hutembelea vivutio mbalimbali," alisema Ndaweka.

Wadhamini wa Kilimanjaro Marathon 2022 ni Kilimanjaro Premium Lager, Tigo, Grand Malt, Absa, Unilever, Kiwanda cha Sukari TPC, Simba Cement, Maji ya Kilimanjaro, GardaWorld Security, hoteli za Keys, Kibo Palace na CMC Automobiles.



Mkurugenzi wa Ufundi wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Oscar Mirambo (kushoto), akitoa maelekezo kwa washiriki wa kozi ya ukocha ya CAF Diploma C inayoendelea kwenye makao makuu ya shirikisho hilo Ilala, jijini Dar es Salaam. **PICHA: TFF**

# Tamasha la Senene Desemba 22 - 26

**Na Saada Akida**

NAIBU Waziri wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Mary Masanja, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika kilele cha Tamasha la utamaduni la Senene lililopangwa kufanyika kuanzia Desemba 22 hadi 26, mwaka huu kwenye viwanja vya Gymkhana, Bukoba mkoani Kagera.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Customer Satisfaction Developed Limited (CSDL), Emmanuel Mwombeki, alisema lengo la tamasha hilo ni kudumisha sanaa na utamaduni wa watu wa mkoa wa Kagera.

Mwombeki alisema katika tamasha hilo pia kutakuwa na shughuli mbalimbali ikiwamo mbio za kilomita 10, matembezi ya hisani, kazi za ujasiriamali, utunzaji wa mazingira, utalii, burudani ya ngoma za asili, sarakasi, muziki wa dansi na kizazi kipya.

Alisema mbali na michezo kutakuwa na fursa ya kupata ladha adimu ya vyakula vya asili kutoka kwa makabila ya mkoa huo pamoja na majirani zao Mwanza.

Naye Meneja wa Programu kutoka CSDL, Beatrice Millinga, alisema wamejipanga kuhakikisha wanaenzi utamaduni na utalii wa hapa nchini huku akiongeza wameandaa mafunzo ya kuwapa uwezo kwa watoa huduma ya kuongoza watalii.

"Kazi yetu kubwa ni kutoa elimu elekezi kwa wadau wa chini na kati ili kuboresha huduma zao kwa wateja hasa kwa watalii, tunatarajia tamasha ya Senene litachangia kuleta mabadiliko," alisema Millinga.

## Waluguru Original waalikwa Dodoma

**Na Sabato Kasika**

BENDI ya Waluguru Original yenye maskani yake Morogoro imepata mwaliko wa kushiriki onyesho maalum liitwaalo 'Wafia Dansi' litakalofanyika Desemba 4, mwaka huu, jijini Dodoma, imefahamika.

Onyesho hilo la nne kwa mwaka huu litashirikisha bendi tano ambazo ni Twanga Pepeta, CP Academia, Bogos kutoka jijini Dar es Salaam, Mjengoni Classic kutoka Arusha na wenyeji Sky Melody.

Mkurugenzi wa Waluguru Original, Killer Boy, aliliambia gazeti hili amefurahi kupata mwaliko huo ambao anaamini utawasaidia kuitambulisha bendi yao katika jiji hilo ambalo sasa ni makao makuu ya nchi.

"Hii itakuwa ni mara ya tatu bendi yetu kushiriki kwenye onyesho hilo lenye lengo la kuimarisha muziki wa dansi nchini, " alisema Killer Boy.

Mkurugenzi huyo alitaja baadhi ya nyimbo za albamu yao mpya watakazozitambulisha katika tamasha hilo 'Morogoro Yetu, Mwanzo wa Mapenzi, Cha Kupewa, Ngalile Mwanangu Ndole, Supu na Nataka Nilewe'.

## Mastraika chanzo Mtibwa kudidimia

**Na Adam Fungamwango**

UONGOZI wa Mtibwa Sugar ambayo inaburuza mkia kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara umesema sababu kubwa ya timu yao kupata matokeo mabaya ni kiwango cha chini kinachoonyeshwa na mastraika wake.

Ofisa Habari wa Mtibwa Sugar, Thobias Kifaru, alisema bado hawajaridhishwa na safu ya ushambuliaji na wanaahidi kuifanyia maboresho wakati wa dirisha dogo.

Kifaru alisema Kocha Mkuu, James Omog amekuwa akiwalalamikia washambuliaji wake na kuweka wazi wanakosa umakini wanapokaribia lango la timu pinzani, hivyo kupoteza nafasi za kufunga wanazozitengeneza.

"Kilio kikubwa kwa Omog ni safu yake ya ushambuliaji, anawalalamika hawako makini wanapokaribia lango. Nikiri hilo ni la kweli, mastraika wetu wametuangusha sana," alisema Kifaru.

Kwa misimu mitatu sasa, Mtibwa Sugar, Mabingwa wa Tanzania Bara mwaka 1999 na 2000, wamekuwa hawafanyi vizuri na msimu uliopita ilinusurika baada ya kushinda mechi za mchujo.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MESSI: SIRUDI BARCA

NYOTA wa PSG, Lionel Messi, 34, hana mpango wa kurudi Barcelona baada ya Rais Joan Laporta kusema klabu hiyo ya Hispania inaweza kumsajili raia huyo wa Argentina katika siku za usoni. ***(AS)***

### POCHETTINO ANUKIA UNITED

KOCHA wa Paris St-Germain na raia wa Argentina, Mauricio Pochettino ndio mkufunzi namba moja anayenyatiwa na klabu ya Manchester United ili kuchukua kazi hiyo msimu ujao. ***(Mail)***

### HAG ATAJWA TRAFFORD

KOCHA wa Ajax na raia wa Uholanzi, Erik ten Hag yupo katika nafasi ya pili miongoni mwa wakufunzi wanaotafutwa na Manchester United ili kuchukua nafasi ya Ole Gunnar Solskjaer, ambaye ametimuliwa. ***(Sky Sports)***

### HAG AAMUA KUFUNGUKA

TEN Hag amejibu uvumi kwamba, atachukua nafasi ya Ole Gunnar Solskjaer katika klabu ya Manchester United kwa kusema hajasikia ombi lolote kutoka kwa klabu hiyo. ***(Manchester Evening News)***

### LOPETEGUI APIGIWA CHAPUO

WAKALA Jorge Mendes anaisukuma Manchester United kujaza pengo la Ole Gunnar Solksjaer kwa kumwajiri kocha wa Sevilla, Julen Lopetegui. Raia huyo wa Hispania ana mkataba na klabu hiyo hadi mwaka 2024, lakini Mendes ambaye anamwakilisha, Cristiano Ronaldo anamtaka kuchukua kazi hiyo. ***(Manchester Evening News)***

### ENRIQUE AIKANA UNITED

KOCHA wa Timu ya Taifa ya Hispania, Luis Enrique, amekana madai yanayomhusisha na mchakato wa kujiunga na Manchester United inayoshiriki Ligi Kuu England. ***(Goal)***

### MADRID YAMTAKA MOUNT

REAL Madrid imeweka wazi nia yake ya kumsajili kiungo wa Chelsea na Timu ya Taifa ya England, Mason Mount (22). Mchezaji huyo yupo katika mazungumzo na klabu hiyo kuhusu mkataba mpya, ingawa inasemekana anahisi hapendwi na huenda akajiandaa kuondoka. Manchester City na Bayern Munich pia zinahusishwa naye. ***(Fichajes)***

### BARISIC ANUKIA VILLA

KOCHA mpya wa klabu ya Aston Villa, Steven Gerrard anataka kumsajili beki wa kushoto wa Timu ya Taifa ya Croatia, Borna Barisic, 29, kutoka klabu yake ya zamani Rangers. ***(Daily Record)***

### BENITEZ AANZA MIPANGO

KOCHA wa Everton, Rafael Benitez amesema klabu hiyo itahitaji kuwasajili wachezaji wapya katika dirisha la uhamisho la Januari, huku winga wa England, Demarai Gray, 25, akiwa mchezaji wa hivi karibuni kupata jeraha wakati wa mechi waliyopoteza kwa Manchester City. ***(Liverpool Echo)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# POCHETTINO: NAWEZA KUJIUNGA NA UNITED

●●● Lakini asema kwa sasa si wakati mwafaka wa kulizungumzia suala hilo...

**PARIS,** Ufaransa

MAURICIO Pochettino amekataa kuondoa uwezekano wa yeye kuwa kocha ajaye wa Manchester United baada ya Paris Saint-Germain kufungwa na Manchester City.

Vinara hao wa Ligue 1 walianza kuongoza katika mechi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa Etihad, lakini mabao kutoka kwa Raheem Sterling na Gabriel Jesus yaliiwezesha City kuibuka na ushindi wa magoli 2-1 na kupaa kileleni katika Kundi A kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya hapo juzi Jumatano.

**Mechi hiyo ilitawaliwa na kivuli kuhusu uvumi wa Pochettino ambaye ni kocha wa zamani wa Tottenham kutajwa kupewa nafasi ya kurithi mikoba ya Ole Gunnar Solskjaer hapo United.**

Licha ya kusisitiza kabla ya mchezo huo ana furaha kuwa PSG, uvumi umeendelea kumhusisha raia huyo wa Argentina kuchukua nafasi ya ukocha kwenye viunga vya Old Trafford. Akizungumza baada ya mchezo huo jijini Manchester, Pochettino alishindwa kuondoa uwezekano wa kwenda kuiongoza Manchester United.

"Wachezaji wote wanafahamu kuhusu hali hii," alisema akinukuliwa na L'Equipe.

"Kuna uvumi kuhusu mazingira haya, mengine ni chanya, mengine ni hasi. Sasa si wakati wa kuzungumzia kuhusu hilo."

MECHI KALI
HOME
AWAY
RUVU SHOOTING
2.64 | 2.59 | 2.98
KAGERA SUGAR

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 710

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# GUARDIOLA AKUNWA NA KIWANGO AKIIVAA PSG



**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amekisifia kikosi chake kwa kiwango bora wakati wakifuzu hatua ya 16 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya kuifunga Paris Saint-Germain 2-1, juzi Jumatano.

City itamaliza ikiwa kileleni katika Kundi A, na imekuwa timu ya pili kutoka England kukaa kileleni mwa kundi katika misimu mitano mfululizo kwenye mashindano hayo.

City walianza kuwa nyuma kwa bao la Kylian Mbappe kabla ya Raheem Sterling na Gabriel Jesus kufunga mabao mawili na kuiwezesha timu hiyo kupata ushindi.

"Tulicheza vizuri sana na tulikuwa tumeonyesha kiwango cha kuvutia," alisema Guardiola akiwaambia waandishi wa habari.

Manchester City licha ya kucheza bila ya Kevin De Bruyne, Jack Grealish na Phil Foden, huku Oleksandr Zinchenko akipewa nafasi ya tatu kuanza msimu huu, walionyesha kiwango cha kuvutia.

# *Ancelotti asifia kiwango cha Kroos*

**MADRID,** Hispania

CARLO Ancelotti amemsifia kiungo, Toni Kroos baada ya kuonyesha kiwango cha kuvutia wakati Real Madrid ikishinda mabao 3-0 dhidi ya Sheriff katika Ligi ya Mabingwa Ulaya iliyochezwa juzi Jumatano.

Kroos alifunga bao la pili kwa Los Blancos baada ya David Alaba kufunga la goli la ufunguzi, huku Karim Benzema akiongeza la tatu kipindi cha pili.

Ushindi huo uliwasaidia miamba hao wa LaLiga kutinga hatua ya 16 kwenye michuano hiyo ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kroos sasa amehusika katika mabao manne katika mechi tatu zilizopita za mashindano yote kwa Madrid (mabao mawili, asisti mbili) - na Ancelotti amefurahishwa na mchango wake huo.

"Kama Kroos akiwa vizuri kocha anatulia," alisema Ancelotti, ambaye ni raia wa Italia. "Ana uwezo wa kumiliki mpira kuliko mtu yoyote.

"Muunganiko wa Casemiro na Modric ni wa aina yake. Pia anafunga mabao na anafanya vizuri sana."



,494,580

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 27/11/21 | 18:00 | Crystal Palace vs Aston Villa | 2.18 | 3.30 | 3.35 |
| 02. 27/11/21 | 18:00 | Hull City vs Millwall | 2.70 | 3.09 | 2.60 |
| 03. 27/11/21 | 18:00 | Huddersfield vs Middlesbrough | 2.46 | 3.10 | 2.85 |
| 04. 27/11/21 | 20:00 | Juventus vs Atalanta | 2.22 | 3.46 | 3.12 |
| 05. 27/11/21 | 20:30 | Mallorca vs Getafe | 2.43 | 2.90 | 3.30 |
| 06. 27/11/21 | 20:30 | Cercle Brugge vs Mechelen | 2.66 | 3.45 | 2.44 |
| 07. 27/11/21 | 20:45 | Fortuna Sittard vs Groningen | 2.72 | 3.26 | 2.47 |
| 08. 27/11/21 | 23:00 | Villarreal vs Barcelona | 2.69 | 3.33 | 2.57 |
| 09. 28/11/21 | 15:30 | Nurnberg vs St. Pauli | 2.60 | 3.23 | 2.60 |
| 10. 28/11/21 | 17:00 | Brentford vs Everton | 2.38 | 3.20 | 3.05 |
| 11. 28/11/21 | 17:00 | Bordeaux vs Brest | 2.42 | 3.34 | 2.84 |
| 12. 28/11/21 | 18:15 | Espanyol vs Real Sociedad | 3.30 | 3.25 | 2.22 |
| 13. 28/11/21 | 18:30 | Maritimo vs Pacos Ferreira | 2.66 | 3.10 | 2.66 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 26 - NOVEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:30 | 1267 | NK Sesvete vs Rudes Zagreb | 2.65 | 3.03 | 2.55 |
| 15:30 | 5252 | Slavia Sofia vs Botev Plovdiv | 2.12 | 3.18 | 3.18 |
| 15:45 | 2933 | IA Sud America vs CA Rentistas | 2.84 | 3.22 | 2.29 |
| 16:00 | 1274 | National Bank vs Arab Contractors | 2.41 | 3.16 | 2.91 |
| 16:00 | 1560 | Hapoel Raanana vs AS Ashdod | 2.67 | 3.06 | 2.72 |
| 16:00 | 2128 | Ahi Nazareth vs Maccabi Bney Reine | 2.36 | 3.12 | 3.07 |
| 16:00 | 3576 | Ruvu Shooting vs Kagera Sugar | 2.64 | 2.59 | 2.98 |
| 16:00 | 4157 | Hapoel Petah Tikva vs Hapoel Ramat Gan | 2.44 | 3.03 | 3.03 |
| 16:00 | 4312 | Hapoel Acre vs Beitar Tel Aviv Ramla | 2.14 | 3.18 | 3.48 |
| 16:00 | 4345 | Ironi Hasharon vs Hapoel Rishon Lezion | 2.48 | 3.08 | 2.93 |
| 17:00 | 3893 | FC Goa vs Jamshedpur | 2.15 | 3.33 | 2.99 |
| 17:30 | 2583 | Balikesirspor vs Manisa BBSK | 5.79 | 4.15 | 1.46 |
| 17:45 | 2664 | Cherno More vs Beroe | 1.92 | 3.32 | 3.61 |
| 17:50 | 5747 | Al Taawon vs AL Faiha | 1.78 | 3.67 | 4.27 |
| 18:00 | 1428 | Jihlava vs Usti Nad Labem | 2.17 | 3.03 | 3.22 |
| 18:00 | 2907 | Inter Zapresic vs Dinamo Zagreb II | 2.31 | 3.07 | 2.93 |
| 18:30 | 3534 | Hermanstadt vs Petrolul Ploiesti | 2.55 | 2.98 | 2.69 |
| 18:30 | 4768 | Ismaily SC vs Ghazl EL Mahallah | 1.89 | 3.35 | 4.04 |
| 19:00 | 3968 | Senica vs MSK Zilina | 3.57 | 3.62 | 1.84 |
| 19:40 | 4745 | Al Ahli Jeddah vs Al Nasr Riyadh | 3.13 | 3.47 | 2.16 |
| 20:00 | 1704 | Genclerbirligi vs Bursaspor | 2.32 | 3.43 | 2.66 |
| 20:00 | 2018 | Crotone vs Vicenza | 2.10 | 3.29 | 3.34 |
| 20:00 | 2570 | NK Osijek vs Lokomotiva Zagreb | 1.54 | 3.96 | 5.02 |
| 20:00 | 3879 | Ethnikos Achnas vs Olympiakos Nicosia | 3.27 | 3.47 | 2.10 |
| 20:00 | 5325 | Basaksehir vs Altay | 1.75 | 3.59 | 4.43 |
| 20:00 | 5477 | Adana Demirspor vs Kasimpasa | 2.00 | 3.50 | 3.45 |
| 22:00 | 1201 | ADO Den Haag vs Dordrecht | 1.21 | 6.27 | 9.79 |
| 22:00 | 1272 | FC Oss vs Telstar | 2.24 | 3.51 | 2.83 |
| 22:00 | 1515 | NEC Nijmegen vs Cambuur | 2.10 | 3.49 | 3.15 |
| 22:00 | 1785 | Roda Kerkrade vs VVV Venlo | 1.42 | 4.69 | 6.05 |
| 22:00 | 2097 | De Graafschap vs Jong Ajax | 1.68 | 4.19 | 4.00 |
| 22:00 | 2690 | Hajduk Split vs Istra | 1.29 | 4.99 | 7.86 |
| 22:00 | 3912 | FC Volendam vs Den Bosch | 1.29 | 5.49 | 7.65 |
| 22:00 | 5241 | FC Eindhoven vs Jong AZ Alkmaar | 1.78 | 3.86 | 3.81 |
| 22:00 | 5488 | Maastricht vs Jong PSV | 3.07 | 3.66 | 2.06 |
| 22:00 | 5689 | SBV Excelsior vs Jong Utrecht | 1.45 | 4.60 | 5.67 |
| 22:30 | 1776 | Lecce vs Ternana | 1.78 | 3.63 | 4.13 |
| 22:30 | 3009 | OKS Odra Opole vs Podbeskidzie Bie | 4.25 | 3.67 | 1.69 |
| 22:30 | 3985 | Stuttgart vs Mainz | 2.79 | 3.38 | 2.44 |
| 22:30 | 5453 | FC Thun vs SC Kriens | 1.50 | 4.05 | 5.41 |
| 22:45 | 3550 | Cagliari vs Salernitana | 1.93 | 3.66 | 3.71 |
| 22:45 | 4012 | Glentoran Belfast vs Dungannon Swifts | 1.16 | 6.53 | 11.53 |
| 22:45 | 5026 | Colchester vs Newport | 3.14 | 3.24 | 2.21 |
| 22:45 | 5203 | Union Saint Gilloise vs OH Leuven | 1.34 | 5.32 | 7.10 |
| 23:00 | 1210 | West Bromwich vs Nottingham | 1.66 | 3.69 | 4.82 |
| 23:00 | 1535 | Mirandes vs Real Oviedo | 2.75 | 2.95 | 2.65 |
| 23:00 | 3459 | Athletic Bilbao vs Granada | 1.50 | 4.11 | 6.61 |
| 23:00 | 3524 | Alcorcon vs Lugo | 2.50 | 2.94 | 2.94 |
| 23:00 | 3747 | Lens vs Angers | 1.87 | 3.59 | 3.99 |
| 23:15 | 4873 | Moreirense vs Gil Vicente | 2.53 | 3.07 | 2.83 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.



# BENZEMA AKUTWA NA HATIA YA ULAGHAI

**PARIS,** Ufaransa

KARIM Benzema amepatikana na hatia katika kesi ya ulaghai ya mchezaji mwenzake, Mathieu Valbuena.

Benzema alikuwa akishtakiwa nchini Ufaransa kwa kosa la ulaghai kutokana na kashfa ya video ya ngono ambayo ilimfanya afungiwe na Timu ya Taifa ya Ufaransa.

Mshambuliaji huyo wa Real Madrid alishutumiwa kwa kumlaghai mchezaji mwenzake Valbuena kwa kutumia video ya ngono aliyokuwa ameipata kumshurutisha alipie ili isivuje.

Kwa sababu ya sakata hilo, aliachwa nje ya kikosi cha Euro 2016 na Kombe la Dunia la 2018, pamoja na michezo mingine ya Ufaransa baada ya kashfa hiyo.

Benzema alikuwa anashtakiwa Ufaransa, na Mahakama ya Versailles imeamua kupitia mazungumzo kati ya Benzema na Valbuena, akijaribu kumshawishi awasiliane na walaghai hao, yalitokana na jaribio la 'makusudi' kuhakikisha mchezaji mwenzake analipa ili kuzuia kutolewa kwa video.

Kutokana na hali hiyo, Benzema amepatikana na hatia ya "kula njama ya ulaghai".



# Dembele ni mchezaji wa kipekee - Xavi

**BARCELONA,** Hispania

KOCHA wa Barcelona, Xavi Hernandez na mlinzi anayerejea, Dani Alves wanakubaliana na uhalisia kuwa Ousmane Dembele ni mchezaji muhimu na wa pekee ndani ya kikosi chao.

Barcelona inaendelea na mazungumzo juu ya mkataba wa nyota huyo wa kimataifa wa Ufaransa.

Dembele amekuwa akikwama kwenye changamoto ya majeraha tangu alipowasili klabuni hapo kwa uhamisho wa zaidi ya euro milioni 100, akitokea Borussia Dortmund mwaka 2017.

Kutokana na changamoto ya majeraha nyota huyo mwenye umri wa miaka 24 ameshindwa kufikia matarajio ya wengi klabuni hapo.

Hata hivyo, Xavi na Alves wanakiri nyota huyo bado ana umuhimu mkubwa klabuni hapo, na anahitaji kupewa muda ili aweze kufanya vizuri zaidi.

"Dembele kwa nafasi yake anaweza kuwa mchezaji bora duniani. Anahitaji kuwa kwenye viwango kama mchezaji wa kimataifa. Ni muhimu kuwa na mtazamo wa ushindi. Tunahitaji kumsaidia," alisema Xavi.

Alves, akiwa anarejea klabuni hapo alizungumza na vyombo vya habari juu ya mtazamo wake juu ya Dembele.

# Michezo

Ijumaa Novemba 26, 2021

Nipashe




Pochettino: Naweza kujiunga na United

UKURASA 21



Kiungo mshambuliaji wa Simba, Ibrahim Ajib (kushoto), akiwania mpira dhidi ya beki wa timu hiyo, Shomary Kapombe wakiwa kwenye maandalizi ya mechi ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Red Arrows kutoka Zambia itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam. **PICHA: SIMBA SC**

## Kocha Nabi aichambua Mbeya Kwanza FC

**Na Saada Akida**

WAKATI kiungo wa kimataifa wa Yanga, Yannick Bangala ataukosa mchezo wa Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara dhidi ya Mbeya Kwanza kutokana na kadi tatu za njano, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Nasreddine Nabi amewachambua wapinzani wao kwa kusema ni timu iliyojengeka.

Mbeya Kwanza ambayo imepanda daraja msimu huu, itaikaribisha Yanga katika mchezo wa raundi ya saba utakaochezwa Jumanne Novemba 30, mwaka huu kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya.

Nabi aliliambia gazeti hili kikosi chake kinaendelea vyema na maandalizi kuelekea mchezo huo ambao utakuwa na ushindani kwa sababu zinakutana kwa mara ya kwanza kwenye ligi.

Kocha huyo alisema hana wasiwasi na mchezo huo na amejiandaa kutumia wachezaji ambao watapambana kuhakikisha wanapata matokeo mazuri na kuendelea kujiimarisha katika msimamo wa ligi.

"Itakuwa mechi yenye mvuto, tunakutana na timu mpya kwenye ligi, lakina katika soka hakuna udogo, tumejiandaa kuendelea kuwapa furaha mashabiki wetu, tunahitaji ushindi katika kila mechi," Nabi alisema.

Yanga yenye pointi 16 ndio vinara wa ligi hiyo wakifuatiwa na mabingwa watetezi, Simba yenye pointi 14 huku Mtibwa Sugar ikiburuza mkia baada ya kujikusanyia pointi mbili kwenye mechi sita ilizocheza.

# Simba yakamilisha 'mawindo'

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

## ●●● Ni baada ya kunasa mbinu za Red Arrows, ya...

TUMEWANASA! Kauli hiyo imetolewa na benchi la ufundi la Simba kuelekea mchezo wao wa mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Red Arrows kutoka Zambia utakaochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

**Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kocha Msaidizi wa Simba, Thierry Hitimana, alisema wamefanikiwa kupata video za mechi kadhaa za wapinzani wao ikiwamo walipowakaribisha Clube Desportivo 1º de Agosto ya Angola kwenye mashindano hayo msimu huu na kupata ushindi wa bao 1-0.**

Hitimana alisema katika mchezo wa kwanza Red Arrows walionekana wanatumia mfumo wa kujilinda zaidi huku wakifanya mashambulizi ya kushtukiza pale wanapotengeneza nafasi.

Kocha huyo alisema pia walibaini mechi nyingi ambazo Red Arrows walishinda zilitokana na mabao ya mapema na muda uliobakia walitumia kulinda lango lao lisipate madhara.

"Katika mchezo waliocheza ugenini dakika nyingi wanaonekana ni watu wa kuzuia wanapokuwa ugenini jambo ambalo tunatakiwa kuwaandaa wachezaji watakaocheza mchezo wa aina hiyo hali ambayo tulikutana nayo katika mchezo wa ligi dhidi ya Namungo FC," alisema Hitimana.

Alisema pia watacheza kwa tahadhari na kuwaheshimu wapinzani wao ikiwa ni dhana ya kuhakikisha wanafanya vizuri katika mchezo huo ambao wanaanzia nyumbani.

Aliongeza wameshawaandaa wachezaji wao kuhusiana na mbinu hiyo ili kuepuka yaliyojitokeza katika mechi ya marudiano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Jwaneng Galaxy baada ya nyota wao kujiamini na hatimaye wakapoteza mchezo.

"Hata katika maisha umheshimu mpinzani wako na uende naye sawa, sisi tunatakiwa kufanya hivyo ili tufanye vizuri nyumbani kabla ya kwenda ugenini, nina imani sana na wachezaji wangu, Red Arrows tumewaangalia na bado tunaendelea kuwaangalia, sio wabaya, ni timu nzuri sana, tunatakiwa kupambana na kutumia vyema dakika 90 za nyumbani," alisema Hitimana.

Naye Mwenyekiti wa Simba, Murtaza Mangungu amewatoa hofu wanachama na mashabiki wa klabu hiyo kuelekea katika mechi hiyo inayoandaliwa na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Mangungu alisema wamejiandaa 'kisawasawa' si kwenye mechi ya Jumapili tu, bali kwenye michuano yote wanayoshiriki huku akisema lengo ni kuona msimu huu wanafika hatua ya nusu fainali.

"Tumejiandaa vizuri na mechi hii, tunajua michuano hii ni migumu, kwa sababu timu nyingi zinazotolewa kwenye Ligi ya Mabingwa zinapokuja huku, mara nyingi zinazokwenda hadi nusu fainali, fainali na kuchukua ubingwa. Kwa hiyo tumejiandaa kukabiliana na ugumu huo, tunawaomba wanachama na mashabiki wetu wajitokeze waipe nguvu timu yao," Mangungu alisema.

Ofisa Habari Msaidizi wa Simba, Ally Shatry 'Chico' alisema wachezaji wanaendelea vyema na mazoezi, huku Chris Mugalu aliyekuwa majeruhi kwa muda mrefu ameanza mazoezi mepesi.

Hata hivyo hadi kufikia jana mchana, Chico alisema hawafahamu taarifa rasmi za ujio wa wapinzani wao.

"Mara wanasema Alhamisi (jana), mara Ijumaa (leo), lakini sisi tunawasiliana na Shirikisho la Soka Nchini (TFF) kujua ni lini watawasili, kwa upande mwingine tunaendelea na mazoezi, wachezaji wetu wanaonekana wana morali kweli kweli, hasa baada ya ujuo ya kocha mpya, Pablo Franco," alisema Chico.

Wakati huo huo, mchezaji wa zamani wa Yanga, Thabani Kamusoko, raia wa Zimbabwe ameitahadharisha Simba kuwa makini na straika, James Chamanga ambaye ndiye nyota tegemeo wa Red Arrows.

"Siyo timu ya kutisha sana, lakini inacheza kitimu zaidi na inabadilisha mfumo kulingana na timu inayocheza nayo, ina straika wao (Chamanga), ndiye wanamtegemea sana kuwafungia mabao," Kamusoko alisema.

CAF imeruhusu mashabiki wasiozidi 35,000 kuingia uwanjani kushuhudia mchezo huo wa kwanza wa hatua ya mtoano.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 3 0

9 770856 541002 >